# Nipashe

Alhamisi Februari 22, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581594

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
Maoni@guardian.co.tz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




**MAZUNGUMZO MAALUM - 2**

**MJANE WA 'NYAMA YA SWALA' ASEMA HAKIMU ALIYEMHUKUMU ASILAUMIWE**

UKURASA 4

**NCHIMBI** aonya viongozi CCM wasiowajibika



UKURASA 3

**UMMY** aibana NHIF malipo watoa huduma

UKURASA 4

**KORTI** yaelezwa askari wa JWTZ alivyotishia bastola apatiwe bilioni 1/-

UKURASA 5

## MABADILIKO YATIKISA VIGOGO WAKUU KKKT

UKURASA 3

# Risasi zarindima mgogoro ardhi



UKURASA 2

## Uhaba wa sukari kaa la moto

**MA-RC** kitanzini, kibano wanaohujumu chaja...*ukurasa 2*

"Hakikisheni mnashirikiana na Bodi ya Sukari kuwakamata wafanyabiashara wote wanaokwenda kinyume cha maelekezo ya serikali na maelekezo ya Tangazo la Serikali. Pia taratibu za kijinai hasa zinazohusu masuala ya uhujumu uchumi zichukuliwe kwa mfanyabiashara yeyote anayekiuka misingi ya taifa letu." - Mchengerwa



**TANI 100,000**

UKURASA WA 4

## BOT YAONYA UPATU SARAFU MTANDAONI

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imeeleza sababu za kusuasua kuruhusu matumizi ya sarafu mtandaoni kuwa ni upatu wenye ujanja ujanja mwingi ambao wananchi...



## Biashara dawa za kulevya yabainika kwenye masoko

UKURASA 3

**MICHEZO** AWESU RASMI ATAJWA KATIKA RADA ZA YANGA UK. 24

**KATUNI** UK. 6

HABARI KITAIFA

## Nchimbi aonya viongozi wasiowajibika CCM

Na Elizabeth Zaya

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amesema viongozi wanaotokana na chama hicho wanaoshindwa kutimiza wajibu wao wa kutumikia wananchi, siku zao zinahesabika na kwamba hakitawavumilia.

Amesema viongozi wote wanaotokana na CCM wanatarajiwa kuwa watumishi wa wananchi waliowachagua, wakiwatumikia kwa nguvu zao zote, wakiweka maslahi ya umma na Watanzania mbele wakati wote, kabla ya masuala yao binafsi.

Dk. Nchimbi alisema hayo juzi alipokuwa akisisitiza namna bora ya kumuenzi Hayati Balozi Dk. Diodorus Kamala, kupitia salamu za pole na rambirambi za CCM wakati wa kuaga na kutoa heshima za mwisho kijijini kwao Rwamashonga, Jimbo la Nkege, Misenyi mkoani Kagera.

Mbali na salamu za CCM, Balozi Nchimbi pia aliwasilisha salamu maalum za rambirambi kwa wafiwa na waombolezaji wote kisha mkono wa pole kwa familia ya Hayati Dk. Kamala, kutoka kwa Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye alieleza namna alivyoguswa na msiba huo.

Dk. Nchimbi alisema moja ya uwezo mkubwa aliokuwa nao Dk. Kamala ni pamoja na saikolojia ya kutafuta suluhisho la changamoto za watu tangu alipokuwa Rais wa Wanafunzi wa Chuo Kikuu Mzumbe.

Pia alimwelezea kuwa alikuwa mwadilifu, aliyechukia rushwa kwa vitendo, kiasi cha kuwa tayari kugharimu na kupoteza ubunge wa Nkenge katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 kwa sababu hakuwa tayari kupokea fedha kuwasaliti wananchi wa jimbo hilo, aliokuwa anawatetea kwenye changamoto zao.

"Kamala hakuwa mla rushwa. Hili naweza kulisemea kwa kiapo. Hata alipopoteza ubunge, hakuwahi kulalamika kwa sababu alijua zile zilikuwa hela za udhalimu, hela za usaliti kwa wananchi wake. Watu wa namna hii lazima tuwaenzi vizuri kwa kutambua mchango wao mkubwa," alisema Balozi Dk. Nchimbi.

"Hongereni sana Misenyi kwa kuwa na Mwana wa Afrika wa namna hii. Mjisikie fahari sana. Nimefurahi kusikia Mwenyekiti wa Halmashauri na Mbunge wa sasa (Jimbo la Nkenge) walivyoelezea mambo aliyofanya Dk. Kamala na walivyo tayari kuyaendeleza na kufanya zaidi.

"Viongozi tunayo mengi ya kujifunza kwa watu kama Dk. Kamala. Vijana mnayo mengi ya kujifunza kwake hasa kutimiza wajibu kwa kuwatumikia wananchi, kuweka maslahi ya nchi na kuwa na msimamo thabiti bila kigugumizi kwenye maslahi ya nchi. Na sisi CCM wajibu wetu tutawatetea na kuwalinda viongozi wanaotumikia wananchi na kutimiza wajibu wao," alisema.

Kadhalika, Balozi Nchimbi alisema viongozi wachache ambao bado wanasuasua katika kutumikia wananchi, wanatakiwa kuongeza juhudi.

"Wale viongozi wachache wanaotanguliza maslahi yao binafsi mbele, ambao hawatimizi wajibu wao kuwatumikia wananchi, siku zao zinahesabika. Tunatakiwa kuwatumikia wananchi kwa nguvu zetu zote.

"Dk. Kamala alikuwa na msimamo usioyumba kusimamia maslahi ya nchi. Kwenye vikao vya kimataifa, linapokuja suala la kutetea maslahi ya Tanzania, Kamala hakuwa na kigugumizi hata kidogo. Alikuwa na uwezo wa kusema bila kuangalia anaowakatalia wanatoka mataifa gani na watamfikiriaje, alikuwa hamwangalii mtu usoni anatokea wapi. Alikuwa na madhaifu yake kama binadamu lakini yanazidiwa na uwezo na nguvu," alisema.

Dk. Kamala, ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Nkenge kwa nyakati mbili tofauti, kabla ya kuwa Naibu Waziri na Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kisha Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji, Luxembourg na Jumuiya ya Ulaya, mjini Brussels, alifariki dunia Februari 12, mwaka huu.

# Biashara ya dawa za kulevya na pombe zabainika kwenye masoko

Halfani Chusi na Joyce Lameck

BIASHARA ya dawa za kulevya, pombe, kamali na dubwi korokoro zimebainika kufanyika katika soko la Mwenge Coca Cola, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam.

Kutokana na kushamiri kwa biashara hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Kinondoni, Philipo Mwakibete, amepiga marufuku biashara hizo kufanyika katika masoko yote kwenye mamlaka hiyo ya serikali za mitaa.

Katika taarifa yake kwa umma aliyoitoa juzi, Mwakibete amekemea vikali kitendo hicho na kuwataka wanaojihusisha na biashara hizo kuacha mara moja katika Soko la Mwenge Coca Cola, kuanzia siku hiyo.

"Amri unatakiwa kuondoa biashara yako ya kamali, dubwi korokoro, pombe na dawa za kulevya katika eneo la soko la Mwenge Coca Cola kuanzia leo (juzi). Hutakiwi kuonekana katika eneo hilo kwa biashara hizi. Tafadhali upatapo barua zingatia agizo hili," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Waandishi wa habari hii walipomtafuta kwa ufafanuzi zaidi, Mwakibete alisema serikali imefikia uamuzi huo baada ya kupenyezewa taarifa na raia wema kwamba wako wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara hizo.

Alisema biashara hizo ni kinyume cha sheria na miongozo ya masoko, hivyo wameamua kuwaandikia barua ya kuwataka kuacha mara moja.

Mwakibete alikumbusha kuwa maeneo ya soko ni sehemu jumuishi ambayo yanapokea kila aina ya watu na rika tofauti, hivyo uuzaji wa pombe, dawa za kulevya na kamali havileti sifa nzuri kwa wateja hasa watoto."Kwa mfano hapo sokoni tumejenga vyoo vizuri, lakini mtu akilewa anaenda kujisaidia haja ndogo inakuwa kero kwa mtu asiyetumia kilevi," alisema.

Mwakibete alisema kwa wale watakaokaidi hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao, ikiwamo kuwabomolea mabanda na kutumia mamlaka nyingine za kiserikali ikiwamo polisi.

"Ndiyo maana ukiangalia hizo barua zimeenda kwa jina zimewalenga wahusika wanaojihusisha na hizo biashara na kama tutadili, tutadili na mtu kwa jina kwamba siku fulani tulikupa barua umekaidi agizo letu hapo ndipo tutakapoanzia, ukiacha na soko la Mwenge pia, la Msasani wanajihusisha na biashara hii," alisema Mwakibete.

Vilevile aliwataka wafanyabiashara kutoweka biashara ambazo haziruhusiwi kwenye masoko ana kuzingatia sheria.

Mwenyekiti wa Soko la Mwenge, Abdalah Samata, alisema biashara hizo si rafiki kwa ustawi wa soko hilo akiiomba serikali kutilia mkazo.

"Watumiaji wa bangi na pombe wakishalewa wanageuka wanaanza kuleta vurugu, kusumbua wateja na wakati mwingine wanachafua vyoo vya soko kwa kujisaidia ovyo.

Baadhi ya wafanyabiashara sokoni hapo wakizungumza na Nipashe walisema wanakubaliana na uamuzi huo.

Mfanyabiashara Yassin Juma alisema anakubaliana na uamuzi wa serikali kuzuia kamali na dawa za kulevya na kutaka suala la pombe liangaliwe.

"Kama pombe imezuiliwa kwenye soko hili basi iwe nchi nzima na iwe inapatikana katika baa kama ilivyokuwa miaka ya nyuma kwa sababu siku hizi zinapatikana hata kwenye maduka ya mitaani ambako watoto wako," alisema.

"Unakuta mtu anategemea hiyo biashara (pombe) kulea familia na pia wanarudishwa nyuma kiuchumi, sikubaliani na hatua hiyo, ninaunga mkono suala la bangi na kamali," alisema Ally Kiumbe.

Mfanyabiashara mwingine, Martha Mosses, ambaye ni miongoni mwa waliopewa barua za kusitisha biashara ya pombe alisema ametii agizo hilo.

"Hatukuwahi kuitwa katika kikao ili tutoe maoni kuhusiana na suala hili, hata viongozi wa vinywaji wakiitwa kwenye vikao huwa hawapewi nafasi ya kuongea hata kidogo, ndio maana tumekubali walivyotaka wao sawa," alisema.



Mkurugenzi wa Mawasiliano Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mindi Kasiga, akifungua mafunzo ya pili ya viongozi wa vyama vya kitaaluma, yaliyohusisha taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali, yaliyoandaliwa na AICC na JNICC, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJIMSALA**

# Mabadiliko yatikisa vigogo wakuu KKKT

Na Christina Mwakangale

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Gehaz Malasusa, ametangaza mabadiliko ya uongozi wa muda katika kanisa hilo lenye makao makuu jijini Arusha.

Mabadiliko hayo yanatokana na uamuzi wa Halmashauri Kuu ya Kanisa hilo, iliyokaa Februari 12 na 13, mwaka huu katika Hoteli ya Arusha Corridor Springs jijini Arusha pamoja na mambo mengine uliwasimamisha na kuwapa likizo ya siku 30 katibu mkuu na naibu wake anayeshughulikia fedha na utawala.

Katika barua yake kwenda kwa maaskofu, makatibu wakuu wa dayosisi zote za KKKT, Dk. Malasusa alisema uamuzi huo ni utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa katika kikao.

"Kwamba, Mhandisi Robert Kitundu (Katibu Mkuu) na Loata Mungaya (Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala), wamepewa likizo na mwajiri ya muda wa siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya barua hii (Februari 19, mwaka huu).

"Kutokana na nafasi hizo mbili kuwa wazi, nimewaomba hawa wafuatao kushika nafasi kwa muda; Rogath Mollel, Katibu Mkuu, KKKT Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria (Mwanza) kuwa Kaimu Katibu Mkuu na Adrian Olotu, Mkaguzi Mkuu wa Ndani, GSF (Good Samaritan Foundation -Shirika la Msamaria Mwema) kuwa Kaimu Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala," alisema Askofu Malasusa katika barua hiyo.

Kutokana na mabadiliko hayo, Dk. Malasusa aliwaomba viongozi wote wa kanisa hilo kuwapa ushirikiano maofisa hao waliopewa kushika ofisi kwa muda.

"Kamati ya Utendaji ya Halmashauri Kuu ya Kanisa, itapanga kukutana siku si nyingi kuona na kutunza haya yote pamoja na maamuzi mengine kama yalivyoamuliwa na Halmashauri Kuu," alisema.

Hivi karibuni, chombo kimoja cha habari kiliripoti kuwa Mhandisi Kitundu amengʼolewa katika wadhifa wake kwa madai ya kukabiliwa na tuhuma mbalimbali ikiwamo kuwadharau maaskofu.

Hata hivyo, taarifa ya Mkuu wa Kanisa haikueleza kwa kinagaubaga sababu hasa za watendaji hao wakuu wa kanisa kusimamishwa kwao.

MAZUNGUMZO MAALUM - 2

# Mjane wa 'nyama ya swala' asema hakimu aliyemhukumu asilaumiwe

**Na Francis Godwin,** IRINGA

JANA katika sehemu ya kwanza ya mazungumzo haya, Maria Ngoda alieleza namna faraja kutoka kwa wafungwa wenzake na askari wa Jeshi la Magereza zilivyomfanya abadili kusudio lake la kujiua akiwa gerezani baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka 22 gerezani.

Novemba 3, mwaka jana, mjane huyo alihukumiwa kifungo hicho baada ya kukutwa na hatia ya kukamatwa akiwa na vipande 12 vya nyama ya swala, hukumu iliyozua mjadala mkali kitaifa, hata kukatiwa rufani.

Maria, katika mazungumzo na Nipashe juzi, alisema wapo watu wanamlaumu hakimu aliyetoa hukumu, lakini yeye haoni kosa kwa hakimu huyo.

Alisema makosa yako kwake (Maria) kwa kukiri kutenda kosa kutokana na kile alichodai kuelekezwa kufanya hivyo na waliomkamata; walimtaka akubali yaishe, hakimu akatoa hukumu kutokana na mshtakiwa kukiri kutenda kosa.

"Ukweli niliutoa mimi mahakamani, hivyo hakimu asilaumiwe, zaidi ya kumwombea kwa Mungu mambo yake yazidi kunyoka kwani hana kosa lolote," alisema Maria.

Akizungumzia mazingira ya kukamatwa kwake Maria alidai kuwa wakati anakamatwa, alikuwa jirani na ndoo ambayo aliachiwa na mtu anayeitwa Fute ili "amtazamie" na hakujua ndani mna nini, ghafla walitokea watu ambao ni askari pamoja na mwenyekiti wa mtaa ambao walikuwa wakimvizia Fute, lakini mtuhumiwa huyo wa uhalifu aliwashtukia na kukwepa mtego huo, akitelekeza mzigo huo kwa mjane huyo.

"Walipofika eneo la tukio waliuliza 'mwenye ndoo hii ni nani?' Niliwaambia '...ni Fute katoka kidogo'. Wakaniomba nifunue mfuniko wa ndoo, baada ya kufunua..., eneo la tukio walibaki watu wengine, mimi na wao tuliondoka kwenda kwa Fute japo nyumbani hatukumkuta ila mazingira ya kwake tulikuta yakiwa na vielelezo vya nyama pori.

"Baada ya kutoka hapo, tulikwenda nyumbani kwa mwanamke mmoja ambako tulikuta nyama nyeusi ikiwa imechomwa kwa ajili ya kuuza waliichukua na kupakia kwenye gari bila mhusika huku wakijisemesha 'Maria atakwenda kuisaidia Jamhuri' kisha walifika eneo la ndoo na kuniambia nipakie ndoo kwenye gari na kwenda polisi huku wakinitaka nikiri kosa kuwa nyama ile ya swala ni yangu. Kwa kweli niliumia sana."



Maria aliwashukuru Mawakili wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) ambao walimsaidia kutoka gerezani, akitoa shukrani mahususi kwa Mwanaharakati Vitus Nkuna ambaye alisambaza taarifa ya hukumu yake iliyopelekea makundi mbalimbali kuonesha kuguswa na kuanza kumsaidia wakiwamo UWT pamoja na waandishi wa habari kwa umoja wao, akisisitiza kuwa alipata faraja kubwa.

"Huyu Nkuna simjui tu ila nilitamani kukutana naye hata nikambeba mgongoni maana sina zawadi nyingine ya kumpa ila nikiwa gerezani alikuja MNEC Salim Abri (Asas) na kuniulizia 'yule mama aliyefungwa miaka 22 yuko wapi?

Niliishia kumtazama lakini nilitamani kumpa mkono ila taratibu za Magereza hazikuruhusu mimi kumpa mkono wa pongezi, hivyo ninatafuta siku nikutane naye ili kumshukuru na kumwomba yeye na Rais Samia Suluhu Hassan wanisaidie kunijengea nyumba ya kuishi maana sina nyumba ya kuishi," alisema Maria.

Pia alisema kuwa kwa sasa anatamani kufanyabiashara ndogo itakayomwingizia kipato kwa kuwa biashara yake ya awali ilikuwa kuponda kokoto au kuuza mboga za majani mitaani, lakini sasa anatamani kufungua kioski cha bidhaa mbalimbali.

Maria pia aliwashukuru wadau mbalimbali ambao wameendelea kumsaidia na kuahidi kumsaidia mtaji ikiwamo Taasisi ya Sauti ya Haki Tanzania pamoja na Kampuni ya Uwakili ya BLS ambao walijitokeza kumsaidia.

# BoT yaonya upatu sarafu mtandaoni

**Na Salome Kitomari**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imeeleza sababu za kusuasua kuruhusu matumizi ya sarafu mtandaoni kuwa ni upatu wenye ujanja ujanja mwingi ambao wananchi wanapaswa kuwa makini, vinginevyo watalizwa.

Aidha, BoT imesema inaendelea na utafiti wa kina wa sarafu mtandaoni ili kuhakikisha nchi haiingii kwenye mtego wa wajanja na kusababisha madhara ikiwamo sarafu kupotea.

Akiwasilisha hivi karibuni mada ya faida za kutumia njia mbadala za malipo badala ya pesa taslimu, Meneja Msaidizi wa Kurugenzi ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, Kitengo cha Mifumo ya Malipo wa BoT, Fabian Kasole, alisema ni muhimu kwenda kidijitali kutokana na nchi nyingi kufanikiwa lakini umakini wa hali ya juu unatakiwa.

"Digital Currency' (sarafu mtandao) ni upatu ambao sifa moja ya upatu, mjanja ndiye anafaidika. Ni muhimu wananchi wajue, ukiingia huko kuwa mjanja wewe sio mnjanja inakula kwako, benki zote duniani haziongelei 'digital currency' wala matumizi, bali zinaongelea Central Bank Digital Currency (sarafu ya mtandaoni ya Benki Kuu).

"Tanzania tunafanya utafiti wa Central Bank Digital Currency ya BoT ambayo inakuwa na sifa zote za fedha na inatambulika duniani. Tunahitaji kuwa na akiba ya fedha za kigeni, sasa Digital Currency ni makubaliano ya pande mbili. Unanunua unahifadhi, wajanja waliochukua wamechukua wanafanya maendeleo, siku mfumo ukidondoka na wewe unadondoka,"alisema.

Alitoa mfano wa mzungu aliyekwenda kijijini akatangaza anataka kununu nyani, watu wakaingia msituni wakawaleta akawahifadhi kwenye kibanda, kusanya akawaweka kwenye kibanda, akapandisha bei mara mbili ya aliyonunua awali, watu wakaingia msituni wakatafuta, akaongeza tena bei wakatafuta nyani kwenye misitu hawapatikani.

"Yule mzungu alipandisha bei akapandisha bei kutoka Sh. 2,000 aliyonunua akauza Sh. 5,000 mwishowe akawauza kwa Sh. 4,500 ambayo waliona ni punguzo, kisha akawauza wote akaondoka na fedha kwenda kufanya maendeleo akawaacha na nyani," alisema.

Kasole alisema kwasasa kuhusu BoT haishauri sana wananchi kutumia digital currency bali tunawashauri kuzingatia maelezo ya BoT ambayo yamefanyiwa utafiti wa kina juu ya jambo hilo, kwa wakati huu ambao inaelekea kwenye Central Bank Digital Currency wanaotoa elimu kwa umma.

Aidha, Meneja huyo alisema ni muhimu wananchi wakafanya malipo kidigitali na kuachana na matumizi ya fedha taslimu, ili kupunguza madhara wanayoweza kukutana nayo hasa kwa wakati huu ambao huduma za malipo zimeboreshwa na kurahisishwa.

"Ni vizuri kufanya malipo mbalimbali ya huduma na bidhaa kidijitali badala ya kuchukua fedha taslimu unafanya kwa mtandao. Urahisi wake ni kwamba wateja wanaweza kufanya malipo kutoka mahali popote, wakati wowote bila kubeba pesa taslimu au hata kutembelea eneo halisi,"alisema na kuongeza:

"Ukifanya malipo mtandaoni miamala inakwenda kwa kasi, kurahisisha mchakato wa kulipa na kulipa mara moja, kufuatilia malipo kidigitali ambayo yanarekodiwa kirahisi na hivyo kufuatilia rekodi za miamala, usalama ulioimarishwa kwasababu malipo ya kidijitali kwa ujumla ni salama zaidi kutokana na kuwa na vipengele vya juu vya usalama,"alisema.

Kwa mujibu wa meneja huyo, kuchapisha sarafu ni gharama kubwa kuliko thamani ya sarafu husika hivyo kwa kuingia kwenye malipo ya dijitali maana yake serikali itaokoa gharama nyingi ikiwamo za kusafirisha fedha mikoani, kuzirudisha BoT zilizochakaa, usalama wa watu wanaosafirisha na kurahisisha huduma za kiuchumi kwa wakati.

Aidha, alisema maendeleo ya mifumo ya malipo iliyofikiwa tangu mwaka 1997 hadi sasa, kuna mabadiliko makubwa kutoka hundi kuchukua mwezi mmoja hadi siku na saa chache, benki kuongeza kwa maana ya kwamba mtu anaweza kutuma benki nyingine kwa haraka na kufika.

Pia alisema uvumbuzi wa vijana wa kitanzania waliokuwa wanasoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwenye 'mobile money' ya kampuni ya E-Flusi mwaka 2008, alileta mageuzi makubwa na kwamba SafariCom walikuwa wa kwanza kutekeleza na Tanzania kufuatia baadaye.

Alisema maboresho mengine ni Scan QR Code ambayo mteja akisha scan anafanya malipo kirahisi, na kwamba yote yanakuja kwa ajili ya kuondoa matumizi ya fedha taslimu.

Kasole alisema changamoto kubwa zilizopo ni imani kwa umma kwa matumzi ya mifumo ya malipo, woga/hofu na kutojiamini pamoja na kuongezeka kwa utapeli huku wakiwataka wananchi kuchukua tahadhari.

# Ummy aibana NHIF malipo watoa huduma

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema miongoni mwa mambo yaliyopendekezwa na watoa huduma za afya wakiwamo wamiliki wa hospitali binafsi, ni kwamba Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), uwe tayari kufanya malipo kwa wakati na kuondoa makato.

Kadhalika, Ummy amesema mapendekezo mengine ya watoa huduma hizo ni kwamba iwapo watasalia kutoza bei ya awali kulingana na huduma, NHIF izingatie hayo.

Waziri Ummy aliyasema hayo jana, jijini Dar es Salaam, akitoa majumuisho ya ziara ya Kamati ya Kudumu ya Afya na Masuala ya Ukimwi, ilipotembelea Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI),

"Sekta binafsi juzi imetupa masharti, baada ya ule mgogoro kati yao na NHIF. Kwamba wanaweza wakakubali bei za awali, ila kwanza wasitukate makato ovyo na pili watulipe kwa wakati. Nimemwandikia Katibu Mkuu dokezo," alisema Ummy.

Wakati Ummy akisema hayo, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) ilifikisha kilio kwa waziri huyo kwamba inadai takribani Sh. bilioni 10 ambazo hawajalipwa na NHIF.

"Nimeshtuka kusikia NHIF inadaiwa kiasi hicho, nitasimamia kuhakikisha wanalipa kwa wakati." alisema Ummy.

Mwishoni mwa mwaka jana, wamiliki wa hospitali binafsi nchini walitishia kugomea kutibu wagonjwa wa NHIF, i wapo bei mpya zilizotangazwa na mfuko huo, zitaanza kutumika Januari Mosi, 2024 kama ilivyopangwa.

Kupitia taarifa yao kwa vyombo vya habari, wamiliki hao walisema kitita hicho kilipitishwa na serikali bila kuwashirikisha na kitasababisha hospitali nyingi kufungwa kutokana na kupata hasara.

"Kwa miaka saba sasa tangu gharama mpya zitangazwe hazikuwahi kuboreshwa na ilikuwa matarajio yetu kwamba, NHIF itatangaza ongezeko la gharama za huduma na siyo kupunguza.

"Kwa kuzingatia ukweli huu pamoja na mengine kama ucheleweshaji wa malipo kwa zaidi ya miezi minne, mfumuko wa bei, kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola kwa zaidi ya asilimia 20 ndani ya miaka saba APHFTA (Chama cha Watoa Huduma za Afya Binafsi Tanzania), tumeona tutashindwa," ilisema taarifa hiyo.

Ilisema APHFTA iliwasilisha mapendekezo ya namna ya kuboresha uhai wa mfuko ikiwemo kuitaka NHIF ipitie upya mapendekezo ya kibiashara kwa bidhaa zake vikiwamo vifurushi vya WEKEZA, TIMIZA, NAJALI na vinginevyo.

HABARI / TANGAZO

# Korti yaelezwa askari wa JWTZ alivyotishia bastola apewa bil.1/-

Na Grace Gurisha

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imeelezwa kuwa aliyekuwa askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Sufian Kideku, na wenzake walivyomteka na kumtishia kwa bastola mfanyabiashara Hussein Mohamed kisha kutumia simu yake kuwapigia ndugu zake wakiwataka watumiwe Sh. bilioni moja ili wamwachie.

Aidha, inadaiwa kuwa washtakiwa hao walimweleza Mohamed kuwa anahitajika Kituo cha Polisi kwa mahojiano na alipokaidi kufanya hivyo, walimwibia simu yake aina ya IPhone huku wakijitambulisha kwake kuwa wao ni maofisa usalama wakati si kweli.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mfanyabiashara Celestine Kamuli, mkazi wa Kizuka, Morogoro na Husein Mwinyijuma, mkazi wa Gairo, Morogoro ambaye ni mtumishi wa JWTZ.

Hayo yalielezwa jana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Aaron Lyamuya, wakati akiwasomea washtakiwa hao hoja za awali.

Mwanga alidai kuwa washtakiwa wote wanakabiliwa na mashtaka manne ambayo ni unyang'anyi wa kutumia silaha, kujifanya mtumishi, kuteka na kujaribu kutishia kwa lengo la kujipatia kitu.

Alidai kuwa, Mei 17, 2023, eneo la Zaramo, Mtaa wa Jamhuri, Posta wilayani Ilala, Dar es Salaam, walijitambulisha kwa mfanyabiashara Hussein Mohamed kama maofisa usalama.

Alidai kuwa washtakiwa hao walimweleza Mohamed kuwa anahitajika kituo cha polisi kwa mahojiano na wakati akikaidi kufanya hivyo, walimwibia simu aina ya IPhone.

Mwanga akiendelea kusoma hoja hizo, alidai kuwa washtakiwa hao walimtishia Mohamed kwa bastola kumtaka aingie katika gari aina ya Toyota Mark II nyeusi.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa walitumia simu ya Mohamed kuwapigia ndugu zake wakitaka watume Sh. bilioni moja ili waweze kumwachia.

Pia inadaiwa kuwa ndugu hao walitoa taarifa polisi na kufanikisha kukamatwa kwa washtakiwa na kupelekwa Kituo Kikuu cha Polisi, Dar es Salaam na baadaye mahakamani kujibu mashtaka dhidi yao.

Baada ya kusomwa hoja hizo, washtakiwa kupitia mawakili wao, walizikana tuhuma hizo isipokuwa majina, anwani zao, kukamatwa na kufikishwa mahakamani.

Upande wa mashtaka ulidai kuwa utakuwa na mashahidi 12 na vielelezo mbalimbali wakati wa usikilizwaji wa kesi hiyo. Kesi hiyo iliahirishwa hadi Machi 6, mwaka huu, kwa ajili ya usikilizwaji.

# Biteko atoa maagizo mazito umeme

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ametoa maagizo mbalimbali ikiwamo wataalamu kufanya ukarabati wa miundombinu ya umeme kwa wakati ili kuwawezesha wananchi kupata huduma ya uhakika.

Amesema tabia ya kutobadilisha au kukarabati miundombinu kwa wakati pale inapoharibika inawakosesha wananchi huduma kwa kipindi kirefu.

Biteko alitoa maagizo hayo juzi wakati wa ziara yake mkoani Njombe ambayo pamoja na mambo mengine, aliwasha umeme katika kijiji cha Ikwavila na Shule ya

Sekondari ya Wasichana Njombe iliyoko wilayani Wanging'ombe na kukagua miundombinu ya uzalishaji umeme na nguzo za umeme katika kiwanda cha TANWAT.

Alitoa maagizo hayo baada ya Mbunge wa Wanging'ombe, Dk. Festo Dugange, kueleza kuwa wilaya hiyo ina changamoto ya radi nyingi zinazosababisha transfoma kuungua kwa takribani 50 hadi 60 kwa mwaka lakini ubadilishaji wake umekuwa ukichukua muda mrefu, hivyo kuathiri shughuli za kijamii na kiuchumi.

"Hili suala la transfoma inaungua halafu inachukua hadi mwezi mmoja kubadilishwa. Uzembe huu haukubaliki, idara ya ununuzi TANESCO (Shirika la Umeme Tanzania) tumeibadilisha kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo hii ya uzembe wakati vifaa hivi vinazalishwa kwenye viwanda vya ndani.

Tunataka watendaji hawa waone shida wanazopata wananchi na kuzitatua.

kweli kuna changamoto ya umeme lakini kuna baadhi ya matatizo TANESCO wanaweza kuyamaliza," alisema Dk. Biteko.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan hataki kero ya umeme iendelee ndiyo maana utekelezaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JHNPP) unaenda kwa kasi na sasa umefikia asilimia 97 na mtambo mmoja umekamilika utakaoingiza megawati 235 kwenye gridi mwezi huu huku mtambo mwingine ukitarajiwa kuingiza megawati nyingine 235 mwezi ujao.

Kuhusu ombi la Mbunge wa Wanging'ombe kupata laini ya umeme inayojitegemea kutokana na iliyopo sasa kutumiwa pia na eneo Lupembe na

TANWAT, hivyo kufanya umeme kuwa hafifu, aliiagiza TANESCO kujenga kituo cha kupoza umeme wilayani humo ili kutengeneza hali ya upatikanaji umeme.

Dk. Biteko alisema serikali imeamua kwa nia moja kuwaletea maendeleo wananchi kwa kutekeleza miradi katika sekta zote zikiwamo miundombinu, nishati, afya na maji ndiyo maana

Wanging'ombe imesambaziwa umeme kwenye vijiji vyote 108 na zaidi ya asilimia 56 ya vitongoji wilayani humo vimesambaziwa nishati hiyo huku kazi ikiendelea na kwamba Sh. bilioni tisa zimetengwa kwa ajili ya kusambaza umeme wilayani humo.


## Lindi Jumbo Limited

TANZANIA

Lindi Jumbo Limited

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR PROVISION OF SECURITY SERVICES TO THE MINING SITE REFERENCE NO LJL-2024-04 LINDI JUMBO GRAPHITE PROJECT**

**LINDI JUMBO LIMITED** ("the Company") is a registered Tanzanian mining and exploration company currently constructing the Lindi Jumbo Graphite Mine in the Ruangwa District of south-eastern Tanzania. The mine's construction is currently underway and is expected to be completed by Q1 2024, with production anticipated to commence in Q2 2024. We cordially invite experienced and reputable security service providers to express their interest in providing security services for the Lindi Jumbo Graphite Mine.

**BRIEF DESCRIPTION:**
The Company is currently in search of security service providers who have a proven track record of providing reliable and effective security services in the mining industry. We invite expressions of interest from suitably qualified, experienced security service providers who meet our stringent selection criteria.

It is our objective to engage security service provider(s) who have demonstrated a high level of competency in the mining industry. Our company is committed to providing a safe and secure environment for our operations, and we recognize the importance of working with experienced and qualified professionals to achieve this goal.

**REQUIREMENTS:**
We invite companies/organizations which are interested to submit their request in writing. Please ensure that your request includes the following:

1. Updated company profile.
2. Company Code of Conduct and Ethics
3. Copy of Current Business Permit and Trade license
4. Copy of the Incorporation Certificate, the most recent BRELA search, and the latest BRELA application of annual return.
5. Copy of Valid Tax Clearance Certificate (TCC), TIN Certificate and VRN certificate
6. Copy of company memorandum and article of association
7. Compliance with Mining Act-Approved Local Content Plan.
8. Clearance report/statement from the national police department.
9. Capability Statement (A short statement from your bank or recognized financiers demonstrating the company's financial capacity.
10. Copy of certificates of accreditation with other operations.
11. Having adequate experience in providing security to the mining areas
12. List of Insurances.
13. Have maximum professional security specialists on their panel of employees, preferably with a focus on the mining sector.
14. Previous experience in handling stretched operations in mining scenarios across more than three locations.
15. Statement on developing adequate logistics for security services, patrolling, and quick reaction teams, including vehicles and establishment of camps. Good / demonstrated knowledge of local conditions/environment prevailing in the area of operations.
16. Commitment and capability to adhere to the company's high health, safety, security, and environmental standards.
17. Health and Safety Policy
18. Have a training facility and a formal syllabus for the training of the guards, etc.

Companies that have the ability, capacity, and resources to implement the service mentioned above should express their interest by sending together the documents stated in the above section through an email to **info@lj.co .tz** (Max email size 20 MBs); all documents must be submitted in English Language on or before 24:00hrs East African Time (EAT) on **06th March 2024.** The subject of the email should be **"EOI LJL-2024-04-COMPANY NAME".**

Lindi Jumbo Limited will review and assess the documents provided by companies that have expressed interest in accordance with this EOI and conduct evaluations based on internal criteria to determine which companies will be included in the list of pre-qualified companies. Only the pre-qualified companies will receive, by signing a Non-Disclosure Agreement (NDA), an invitation to bid as a continuation of the call for tender process. Lindi Jumbo Limited is not bound to accept the lowest or any tender offer received, and the adjudication of the tender will be based solely on the discretion of the Company, with consideration given to both qualification and commercial aspects.

**Lindi Jumbo Limited (Company No. 124563) Cape Town Fish Market, 3rd floor, Plot No. 180, Msasani Village Block "B" P.O. Box 33773, Dar es Salaam Tanzania Email: info@lj.co.tz Web: www.lindijumbo.co.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio watoa huduma kuhusu NHIF kimefika kwa wakati

**KATIKA** kuhakikisha Watanzania wengi wanapata huduma za afya bila usumbufu na kwa gharama nafuu, serikali ilianzisha bima ya afya kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ma mifuko mingine inayoendeshwa na taasisi binafsi. Lengo la kufanya hivyo ni kuwezesha upatikanaji wa huduma za afya kwa maana ya vipimo na matibabu kuwa rahisi.

Tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000 mfumo huo wa upatikanaji wa huduma za afya umekuwa na unafuu kuliko awali kutokana na ukweli kwamba ni vigumu kwa Watanzania walio wengi kupata matibabu kwa kutumia fedha taslimu kwa sababu uwezo wa kiuchumi wa wananchi wengi ni mdogo. Kwa mantiki hiyo, hivyo ni vigumu kumudu gharama za matibabu ambazo baadhi hugharimu mamilioni ya shilingi.

Licha ya unafuu huo, taasisi zinazotoa huduma za bima ya afya kama vile NHIF, zimekuwa pia zikitoa vivutio kupitia vifurushi vyao na watu binafsi, mashirika na taasisi wamekuwa wakichangamkia ili kuhakikisha watu wao, wakiwamo wafanyakazi na wategemezi wao, wanapata huduma zenye viwango na katika hospitali zenye huduma bora.

Pamoja na nia nzuri ya serikali kuwa Watanzania wengi wapate huduma bora, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya watoa huduma kwamba wamekuwa wakicheleweshwa malipo kutoka NHIF.

Malalamiko hayo yalibainika jana baada ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kubainisha kuwa miongoni mwa mambo yaliyopendekezwa na watoa huduma za afya wakiwamo wamiliki wa hospitali binafsi ni kwamba iwe tayari kufanya malipo kwa wakati na kuondoa makato. Waziri Ummy aliyasema hayo wakati akifanya majumuisho ya ziara ya Kamati ya Kudumu ya Afya na Masuala ya Ukimwi, ilipotembelea Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Dar es Salaam.

Ummy alibainisha kuwa watoa huduma hao wamelalamikia pia makato yanayofanywa na NHIF ambayo yamesababisha mgogoro baina ya pande hizo huku watoa huduma wakisema kitendo cha kucheleweshewa malipo licha ya kuwasilisha madai kwa wakati kinasababisha utoaji huduma kuwa na matatizo.

Kilio hicho cha watoa huduma kimefika kwa wakati na mhusika halisi aliyepewa dhamana ya kusimamia sekta ya afya ambayo pamoja na mambo mengine, inahusika na matibabu kwa wananchi.

Ni wazi kwamba watoa huduma, kwa maana ya vituo vya kutolea huduma za afya vya serikali na binafsi, vimekuwa na mchango mkubwa katika kuhakikisha wananchi wanapata matibabu kupitia bima ya afya. Kwa ujumla, vituo hivyo vimerahisisha sana kuwapo kwa matibabu lakini ucheleweshaji wa malipo kutoka NHIF ni kikwazo kwa maendeleo ya kitaasisi.

Vituo hivyo vimewekeza na vinatumia fedha nyingi kwa ajili ya kufanikisha huduma, hivyo inapotokea ucheleweshaji wa malipo baada ya kuwasilisha madai kutokana na mikataba, lazima vitaathirika na hatimaye kushindwa kutoa huduma zinazostahili.

Pia ikumbukwe kwamba vituo hivyo, hasa vinavyomilikiwa na taasisi binafsi na mashirika ya dini, vina wafanyakazi ambao kipato chao kinatokana na huduma za matibabu kwa wagonjwa, hivyo kunapotokea kukosa fedha, wanashindwa kuendesha maisha yao na matokeo yake kukosa ari ya kufanya kazi.

Matokeo yake, kama msemo wa wapiganapo tembo au wafanyapo furaha nyasi ndizo ziumiazo, vivyo hivyo wafanyakazi ndio waumiao. Pia wamiliki wanaumia kwa sababu wanapata hasara, hivyo kushindwa kutoa huduma istahilivyo na mwishowe wanaweza kufunga taasisi hao.

Kama alivyosema Waziri Ummy, ni vyema NHIF ikawajibika ipasavyo katika kuwalipa madai yao watoa huduma ili kuendeleza huduma za afya kwa faida ya wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Ubunifu, anavyopambana Dk.Samia, ndani na nje uwaamshe wanasiasa

**KAMA** kuna wakati mwanasiasa wanatakiwa kuonyesha umahiri wao, ni kipindi cha kujenga uhusiano na taasisi za umma. Hayo ni miongoni mwa yanayoifanya dunia ikabaki sehemu salama na kuongeza tija kwa wananchi.

Kwetu, kumekuwapo safari nyingi za nje ya nchi ambazo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizuru huku na huko bila kuchoka; hivi karibuni kuanzia Vatican hadi Norway, Indonesia, bila kusahau jirani zake kama Kenya na Uganda.

Ziara zake nyingi za Rais zinaelekea kutoa somo duniani, kuwapo Rais mama, anayechapa kazi katika misingi inayounda sura ya umoja duniani, ,matokeo yake mataifa yatanufaika.

Rais Dk. Samia hatakuwa peke yake, ni lazima wanasiasa waige somo lake la ubunifu katika mahusiano kimataifa.

Mama huyo wa taifa, anaendeleza falsafa kimataifa, kila siku anaunda marafiki wapya na wageni kwa ujumla wake.

Katika ujenzi wa diplomasia ni muhimu kuchukua hatua za kuwafikia wote wenye mchango mkubwa kwetu. Uamuzi wa kumtembelea Papa Francisco, Mkuu wa Kanisa Katoliki kule makao makuu, Vatican ni ushahidi serikali ya Rais Samia imedhamiria kujenga na kuimarisha uhusiano bora kigeni.

Kimsingi, ziara hizo zinaleta tafsiri Tanzania inapiga hatua kubwa kimaendeleo, kama ilivyoonekana kutoka Vatican, mdau mkubwa wa maendeleo.

Tunahitaji ushiriki wa mataifa mengine katika maendeleo ya jamii yetu. Kidiplomasia, inatafsiriwa ni lile linaloshirikiana na mengine, ziitengeneza fursa kwa wananchi wao. Dk. Samia amekuwa mtangulizi katika njia hiyo, akiamini serikali inafanya vizuri kimaendeleo kwa kushirikisha wadau wote duniani kwa hali na mali.

Imani yake ni katika kuwafuata viongozi wenzake ili kubadilishana fikra na fursa. Tunaliona hilo, kila ziara yake, inatoka na fursa kidiplomasia.

Kuna wakati nikabadilishana mitazamo na Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Jabir Makame kuhusu hilo. Naye hakuwa mbali, akisisitiza namna diplomasia ina nguvu na ndiyo inayouwezesha uchumi wa nchi, akitamka:

"Nguvu ya uchumi lazima iwahusishe wengine, kuanzia utaalamu na maarifa mengine. Uimara wa diplomasia yetu ya uchumi ndiyo inayofungua fursa na kuvutia uwekezaji na kutoa fursa mpya za nje ya nchi kwa Watanzania na wawekezaji wa ndani katika Sekta mbalimbali.

"Kazi hii hufanywa na Mwanadiplomasia namba moja wa nchi na wasaidizi wake katika diplomasia. Afrika na dunia," anatamka.

Ikumbukwe, katika ziara hizo Rais Dk. Samia anaambatana na wawekezaji wa ndani, wanaotakiwa kutumia fursa hiyo kutafuta majukwaa na fursa za majadiliano na wawekezaji wa nje.

Aidha, wawekezaji hao wa ndani wanawajibika pia kutambulisha fursa za kiuchumi zinazoweza kuwavutia wawekezaji wa nje.

Kimsingi, suala la uwekezaji kutoka nchini, unazingatia sana uhusiano wa ugenini, wawekezaji wa nje wakitolea macho fursa hizo na uimara wa serikali katika kuwasimamia, kuwalinda na kuwatengenezea zaidi wakiwa nchini.

Hapo hapo ndipo, falsafa ya Rais Dk. Samia inatugusa, kwamba uamuzi wake kuwavutia wawekezaji kama ajenda kuu na msimamo wa serikali imara na yenye utayari kuwalinda, kwa hali mali.

Katika muktadha huo, binafsi nauona uamuzi wa Rais Dk. Samia, unaonesha kwamba usiku na mchana anaiwazia Tanzania ndani na katika katika anga ya kimataifa, ifikie uimara kiuchumi.

Kuna sura nyingine anatuachia, hana nafasi kwa malumbano na mataifa ya kigeni, akihakikisha kila kiongozi wa dunia anaelekeza macho na masikio yake nchini.

Leo hii sio siri, viongozi wa nje wanavutiwa na hilo na ndiyo maana wanakuwa wenyeji wake, hata wakashiriki naye vikao vya ndani na hadharani. Vyote vikiwa na majibu yanayomuunga mkono, pia taifa lake.

Hapo tunaingia tena darasani, akionyesha inawezekana kushirikiana na mataifa mbalimbali, ikiwa serikali inao ubunifu juu kwa yanayotakiwa kufanyika.

Je mafanikio ya serikali ya Rais Dk. Samia yana maana gani? Nui wazi inafungua fursa kiuchumi, kuanzia mataifa jirani ya Afrika Mashariki, Afrika, Ulaya na Amerika, yakitumiwa ujumbe kiongozi wa Tanzania anapeperusha bendera ya nchi yake kuleta mafanikio mtabuka kweao na kwa wotei. Ni wakati wa wawekezaji wa nje kukaribisha mitaji yao.

Pili, anawakumbusha Watanzania kuwa serikali yake ina jukumu la kuhakikisha uchumi wake unakua, pamoja na kuwapo changamoto za ndani na nje.

Tatu, anajenga nguvu katika diplomasia ya Uchumi iliyokio ndani ya ushindani mkubwa duniani hata inamlazimu kuongoza jopo lake kwa juhudi na maarifa.

Hapo inajumuisha kuonekana katika mikutano na ziara za ujumbe wa Tanzania, akikutana na viongozi wenzake wakubwa katika kuamua mazito ya sera na mipango ya maendeleo kimataifa. Hapo kuna wahisani na wadau wa maendeleo.

## Jukwaa la maprofesa lajipanga kuinua taaluma

**Na Mwandishi Wetu**

JUKWAA la Maprofesa wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), limejipanga kikamilifu kuhakikisha linachangia kuinua na kuimarisha shughuli zote za kitaaluma, utafiti na huduma za ushauri wa kitaalam.

Madhumuni ya jukwaa hilo ni kuongeza kiwango cha ubora na taaluma na shughuli zinazosimamiwa na chuo hicho kwa maslahi mapana ya taifa.

Azma hiyo imefikiwa kwa pamoja na wajumbe wa jukwaa hilo wakati wa mkutano wake wa tatu uliofanyika Februari 19 hadi Februari 20, mwaka huu katika kampasi ya Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kilichoko Kibaha mkoani Pwani.

Akizungumza wakati wa kufunga jukwaa hilo, kiongozi wa jukwaa ambaye pia ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Taaluma, Utafiti na Huduma za Ushauri wa Kitaalamu, Prof. Deus Ngaruko, alisisitiza kuwa jukwaa hilo ndiyo sehemu pekee ya wanazuoni kukaa na kujadili mambo yao na kufikia mikakati ambayo italeta tija kwa taasisi na taifa.

"Tumejadiliana na kukubaliana mengi lakini kinachotakiwa sasa ni kushirikiana na taasisi, kampuni na wanataaluma wenzetu wote ndani ya chuo na popote duniani katika kuandika na kusimamia miradi itakayosaidia kuinua na kuboresha maisha ya jamii," alisema.

Makamu Mkuu wa Chuo ambaye pia ni mjumbe wa jukwaa hilo, Prof. Elifas Bisanda, aliwataka wajumbe wengine wa jukwaa hilo kuwa viongozi kitaaluma ili kuwa mfano bora kwa wasomi wengine ambao wanaowaangalia kama kioo na dira ya mafanikio.

"Tunapaswa tuwe kioo halisi cha jamii yetu. Tuhakikishe tunaongoza wengine katika kufanya utafiti na kutoa mihadhara yenye tija. Tuwaongoze wanaotutazama katika kutafuta miradi na kusimamia vyema kazi za kitaaluma," alisema Prof. Bisanda.

Prof. Modestus Varisanga, mjumbe wa jukwaa hilo, alisema pamoja na majukumu mengine, Jukwaa la Maprofesa wa OUT huwakutanisha maprofesa wa chuo hicho na kukumbushana wajibu wao kwa jamii.

Alisema hiyo ni kutokana na ukweli kwamba wasomi wanapaswa kufanya utafiti na kuja na majibu ya changamoto zinazoikabili jamii. Alisisitiza wajumbe wa jukwaa hilo kufanya utafiti na kuandaa mihadhara yenye kuibua na kutoa majawabu ya changamoto zilizoko kwenye jamii ili kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.

Mada mbalimbali ziliwasilishwa na maprofesa wa OUT akiwamo nguli wa sheria, Prof. Alex Makulilo, ambaye ni mbobezi katika sheria za teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na mitandao. Mwingine ni Prof. George Oreku, gwiji katika ICT na ulinzi wa mtandaoni (Cyber Security) nchini.

Pia katika kongamano hilo walikuwapo maprofesa washiriki tisa ambao kila mmoja alitoa mchango wa namna Jukwaa la Maprofesa wa OUT linavyoweza kuwa kiongozi katika kutatua changamoto za jamii kwa kushirikiana na wadau wengine, kuendelea kuiunga mkono serikali katika jitihada kubwa inazofanya kuwaletea wananchi maendeleo.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi (kulia), akisalimiana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu, alipotembelea banda la maonyesho la benki hiyo katika mkutano wa pili wa wadau wa sekta ya utalii Zanzibar (Z-Summit), uliodhaminiwa na benki hiyo, jijini Zanzibar. Wanaoshuhudia ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wawekezaji wa Utalii Zanzibar (ZATI), Rahim Bhaloo (wa pili kulia) na maofisa wengine wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Prof. Janabi: Tatizo la umeme halijaathiri huduma Muhimbili

**Na Christina Mwakangale**

WAKATI kukiwa na tatizo la umeme kila kona, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), imesema tatizo hilo halijateteresha huduma hospitalini hapo.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, katika mahojiano maalumu na vyombo vya habari juzi, alisema ufanisi wa kazi katika kituo hicho cha mafunzo na matibabu ya kibingwa Afrika Mashariki, umeendelea kama kawaida.

Hivi karibuni, Bunge liliipa serikali miezi minne hadi Juni, mwaka huu, kuondokana na mgawo wa umeme na kukatika mara kwa mara unaoendelea nchini.

Kuhusu maendeleo ya MNH pamoja na changamoto zake, Prof. Janabi alisema: "Kwa hali ya kawaida basi hapa ingekuwa hali si nzuri kwamba hata miili ingeharibika, majokofu kama yasingefanya kazi.

"Lakini kwa uwekezaji mkubwa hapa Muhimbili ni pamoja na kujipanga katika jenereta zilizo tayari. Muhimbili ni kubwa Afrika Mashariki na ina vitanda takribani 2,200. Ila Muhimbili si kubwa tu kwa eneo yaani vitanda, bali ukitaka mtaalamu yeyote utampata hapa.

"Ukubwa wa hospitali unatokana na huduma, tumeingia katika matibabu ya kibingwa, 'plastic surgery', tunawekea puto watu kuukabili uzito, tunafanya operesheni kubwa. Na hivi karibuni watoto 21 waliokuwa na jinsi tata wamefanyiwa matibabu," alisema Prof. Janabi.

Pia alisema mpango uliopo ni kuipa hadhi MNH kitaifa na kimataifa inayoendana na majengo ya kisasa huku akibainisha kuwa tayari upembuzi yakinifu umefanyika na ujenzi unaanza kwa awamu hususan kwa kuandaa majengo ya kuwahamishia wagonjwa wanaolazwa.

Prof. Janab alisema Muhimbili inabomolewa na kujengwa upya, kwa awamu ambapo watashirikiana na Korea.

"Kazi ilianza Desemba 2023. Mradi huo utajengwa kwa awamu kadhaa na kugharimu takribani Sh. bilioni 700. Kwa kipindi cha miaka ya hivi karibuni yamefanyika mabadiliko makubwa.

"Kwa siku hapa MNH yanaingia magari 5,000 niligundua kwamba watu wanapaki magari. Sasa tunatumia mfumo wa malipo kwa wageni," alisema.

**UPANDIKIZAJI MIMBA**

Kuhusu huduma ya upandikizaji mimba (IVF), Prof. Janabi alisema imekamilika kwa asilimia 100 katika majengo na vifaa na kinachosubiriwa ni kuwapo kwa benki maalum ya kuhifadhi mayai na mabingwa walioko masomoni.

"Kuzungumziwa muda mrefu huduma hii si kitu, ikumbukwe pia kununua vifaa ni kitu kimoja na kuanza huduma ni kitu kingine.

"Tuligundua wakati huo huo inabidi tuanze kusomesha watu. Tunawajengea uwezo watu wa ndani na wengine wamekwenda nje kama Marekani.

"Jengo lipo tayari, vifaa ni asilimia 100 na hapa tutakacholeta si kupandikiza tu, kadri siku zinavyokwenda ubora wa mayai (kwa wanawake) unapungua, lakini tunataka tuwe na vifaa vya kutunzia mayai yao. Leo mwanamke ana miaka 27 lakini hayuko tayari kuzaa, basi aje ahifadhi, baadaye akiwa tayari apandikizwe mimba," alisema.

Bingwa huyo pia alisema wanalenga soko la utalii kwa ambao wanaweza kuja nchini kwa huduma hiyo.

"Tulishatazama namna ya kuwa na mfumo unaotuna umeme, kwa sababu huwezi kuwa na uwekezaji kama huu mkubwa usiwe na umeme. Mfano pamoja na 'frustrations' ya umeme, lakini huwezi kusikia kuna mwili umeharibika.

"Tumechukua tahadhari kuhusu huduma kwa sababu utahitaji kuhifadhi mayai hii na kukabiliana na changamoto za umeme tuna jenereta," alisema.

**ULINZI WA MWILI**

Prof. Janabi alisema mbali na uwekezaji katika huduma za afya kuwa mkubwa nchini, bado jamii ina wajibu wa kulinda afya zao, kuepukana na gharama za matibabu hasa ya kibingwa.

"Lengo ni kuhakikisha ujenzi unaanza, kwa sababu hata kabla sijazaliwa hospitali hii ilikuwapo na matengenezo ya mara kwa mara yamekuwa ni gharama zaidi, lakini hata uwe na hospitali lukuki, usipobadili mtindo wa maisha ni bure, tuanze kubadilika wenyewe.

"Mimi ni mwalimu na bado ninafundisha. Ndio maana ninaeleza kila siku. Sina lengo la kujenga hofu, kwa sababu ukiwa na hofu kinga ya mwili inashuka. Chukulia hivi, binadamu ana mawazo 70,000 kwa siku na bahati mbaya mengi ya mawazo ni hasi, na simu inakuongezea mitazamo fulani.

"Jamii sasa imeegemea katika matumizi ya simu. Utakuta mtu akiamka tu asubuhi, baba, mama, mtoto ni simu na anashinda na simu. Hafanyi mazoezi. Nikigundua mtu ana shida ya moyo kuanzia uchunguzi hadi tiba si chini ya Sh. milioni sita," alisema.

"Binafsi nikifika katika simu naangalia vitu muhimu. Labda dawa hii inatumikaje, unatumia simu kwa faida yako.Nitaangalia kidogo siasa za ndani, nje zinakwendaje. "Lakini huwezi kumwambia mtoto asitumie simu ila unaweza wewe kuanza kubadilika tujifunze. Moja ya tatu ya bajeti ya Tanzania ni magonjwa yasiyoambukiza," alisisitiza.

Alisema asilimia 28 ya vifo ni magonjwa yasiyoambukiza. Hufanyi mazoezi, unakula chakula kupitiliza, unavuta sigara, unakunywa pombe kupitiliza, jambo ambalo linamfanya mtu kujiuliza kama mwananchi amechukua hatua gani kujilinda.

"Itabakia kuilaumu serikali. Ndiyo maana tunahimiza bima. Ila ukiishi kama unavyoshauriwa utaepuka mengi. Waandishi mtoe habari sahihi ili kuelimisha watu wetu," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Mkumbo akoshwa kasi ya ujenzi kituo biashara Afrika Mashariki

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, amepongeza kasi ya ujenzi wa Kituo cha Biashara cha Afrika Mashariki (EACLC), ambacho kinatakapokamilika kitatoa ajira 15,000 za moja kwa moja na 65,000 za muda.

Kituo hicho kilichoko Ubungo eneo la stendi ya zamani ya mabasi ya mikoani, kinatarajiwa kukamilika Juni, mwaka huu na kitakuwa na zaidi ya maduka 220.

Prof. Mkumbo aliyasema hayo juzi Dar es Salaam wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ilipotembelea miradi ya uwekezaji ikiambatana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Alisema kamati hiyo imeshuhudia na kuridhishwa na kasi ya uwekezaji inayofanywa maeneo mawili makubwa ya uwekezaji yaliyoko Kigamboni na Ubungo, Dar es Salaam.

Prof. Mkumbo ambaye ni Mbunge wa Ubungo, alisema baada ya kufika Ubungo, kamati hiyo imeshuhudia mradi mkubwa wa uwekezaji wa kituo kikubwa cha biashara na usafirishaji cha Afrika Mashariki ambacho uwekezaji wake unafikia takribani Dola za Marekani milioni 110 (Sh. bilioni 280 za Tanzania).

Waziri Mkumbo alisema mradi huo ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Julai mwaka huu unakadiriwa kutengeneza ajira za ndani takribani 15,000 jambo ambalo alisema ni la kujivunia.

Alipongeza kasi ya ujenzi wa kituo hicho na kwamba kitakapokamilika kitasaidia kusisimua uchumi kwani wafanyabiashara wengi wa nchi za Afrika Mashariki watakuwa wakija kununua bidhaa nchini Tanzania.

Kituo hicho, alisema kitapanua fursa kwa Watanzania wengi ambapo wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama machinga nao watapata nafasi ya kufanya biashara nje ya jengo hilo.

Alisema kwa Kigamboni wameshuhudia maendeleo ya kiwanda cha uzalishaji wa nyaya za Umeme cha Elsewedy Electric Industrial Complex kinachotarajia kutengeneza ajira za ndani 400 huku 278 kati yao wakiwa wameajiriwa tayari.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Joseph Mhagama, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutengeneza mazingira rafiki ya uwekezaji nchini yanayosababisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza kwenye maeneo mbalimbali bila vikwazo.

Alisema kazi ya kamati anayoiongoza ni kusimamia na kuishauri serikali kuangalia hali ya uwekezaji nchini ambapo kupitia miradi waliyoishuhudia ni imani yao kuwa itapunguza tatizo kubwa la kuagiza bidhaa nje ya nchi.

Kwa sasa, alisema nchi imekuwa ikinunua zaidi bidhaa kutoka nje ya nchi kuliko kuuza hali inayosababisha kupoteza fedha nyingi za kigeni.

Mkurugenzi wa Kampuni ya East Africa Commercial & Logistics Center, Cathy Wang, alisema kampuni yao inajenga kituo hicho cha kimkakati kitakachoongoza Afrika Mashariki kwa ajili ya biashara za huduma na bidhaa kwa kunakili bidhaa za China kwenye soko la Yiwu na Dubai DragonMart na kuzileta hapa Tanzania.

Alisema kituo kitawezesha kukuza biashara ndogo nchini na kupanua biashara hizo ndani ya soko kubwa la Afrika.




Mkurugenzi wa Shirikisho la Wenye Viwanda Nchini (CTI), Leodegar Tenga, akizungumza kwenye mkutano wa kutangaza maonyesho ya kimataifa ya wazalishaji Tanzania (TIME EXPO 2024), katika ofisi za Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE.**

## Mapendekezo ya Mpimbwe kuwa wilaya

**Na Munir Shemweta,** KATAVI

KAMATI ya Ushauri ya Maendeleo ya Mkoa wa Katavi (RCC) imependekeza Halmashauri ya Mpimbwe kuwa wilaya kamili. Kwa sasa Mpimbwe ni halmashauri ndani ya Wilaya ya Mlele.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambaye ni Mbunge wa Kavuu katika Halmashauri ya Mpimbwe, alishiriki kwenye kikao hicho kilichofanyika juzi katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi.

Kikao hicho mbali na mambo mengine, kilijadili na kupitisha bajeti ya mkoa wa Katavi pamoja na halmashauri zake kwa kipindi cha mwaka 2024/25 sambamba na kupitia maeneo ya utawala.

Naibu Waziri Pinda yuko mkoani Katavi ambapo mbali na shughuli nyingine atashiriki katika Mkutano Mkuu wa Jimbo la Kavuu kwenye Halmashauri ya Mpimbwe mkoani Katavi.

Mkutano huo utafanyika keshokutwa katika Shule ya Sekondari Mizengo Pinda, Kibaoni na utajadili Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya CCM kuanzia Novemba, 2020 hadi Februari, 2023 itakayowasilishwa na Naibu Waziri huyo.

Mgeni rasmi katika mkutano huo anatarajiwa kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambaye ni Mbunge wa Kavuu katika Halmashauri ya Mpimbwe, alishiriki kwenye kikao hicho kilichofanyika juzi katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi.**

# Wenye viwanda, wazalishaji 500 kushiriki maonyesho Dar

**Na Restuta James**

WENYE viwanda na wazalishaji zaidi ya 500 kutoka ndani na nje ya nchi wanatarajiwa kushiriki katika maonyesho ya kimataifa ya viwanda, yanayotarajiwa kufanyika Dar es Salaam Septemba, mwaka huu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa CTI, Leodegar Tenga, alisema jana kuwa maonyesho hayo yatawakutanisha wenye viwanda na wanaokusudia kuingia kwenye uwekezaji huo ili waone teknolojia na uvumbuzi mpya.

"Yataainisha maeneo muhimu ya kiuwekezaji, zana, bidhaa na huduma mpya nchini. Maonyesho ya mwaka jana yalionesha namna ambavyo tunapiga hatua katika ubunifu ikiwamo gari la umeme lililoundwa hapa ndani," alisema Tenga.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), Mkurugenzi wa Kuendeleza Biashara, Fortunatus Mhambe, alisema maonyesho hayo ni uwanja wa kuwakutanisha wazalishaji na wanunuzi na kuwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kushiriki.

"Kutakuwa na viwanda vya bidhaa za ujenzi, vyuma, madini na plastiki, kilimo, rangi, nguo na mavazi, vipodozi, bidhaa za walaji, dawa, teknolojia ya nishati mbadala, umeme, zana za kisasa za viwandani na mashine mbalimbali," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Kaypee Motors, Masoud Kipanya, alisema ili nchi ipate maendeleo haraka inahitaji uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya uzalishaji ambayo itaingiza bidhaa kwenye soko la dunia.

Alisema Tanzania ina fursa nyingi ya kuanzisha viwanda kwa kuwa kuna malighafi za kutosha, mazingira bora na uhakika wa soko kwa kuwa bidhaa nyingi zinaagizwa kutoka nje ya nchi.

"Tuisaidie nchi yetu iwe mzalishaji badala ya kuwa gulio. Inasikitisha kuona kwamba tunauza kidogo sana nje tena malighafi, hali hii ikiendelea tutachelewa sana kukuza uchumi wetu. Ni aibu kwamba tunaruhusu hadi mitumba chakavu ya vitu mbalimbali ambavyo tungeweza kuvizalisha wenyewe," alisema.

Maonyesho hayo yataongozwa na kaulimbiu Kujenga Madaraja: Kuunganisha wazalishaji wa ndani na wa kimataifa.'



# Mradi wa uchimbaji madini tembo waiva

**Na Oscar Assenga,** PANGANI

MRADI wa ubia wa uchimbaji na uchakataji wa madini ya tembo, yanayopatikana kwa wingi Wilaya ya Pangani mkoani Tanga, utaanza kutekelezwa muda wowote kuanzia sasa.

Hatua hiyo ni baada ya serikali kueleza iko katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za leseni kubwa ya uchimbaji wake.

Kampuni ya Nyati Mineral Sands, inayomilikiwa kwa ubia kati ya serikali ya Tanzania na kampuni ya Strandline, zimeingia maktaba wa uchimbaji wa madini hayo.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, aliyasema hayo jana alipokwenda kukagua eneo la utekelezaji wa mradi huo katika Kijiji cha Stahabu, Kata ya Mikunguni, Wilaya ya Pangani.

"Nimefurahishwa na wananchi wanaoguswa na kukubali kupisha kuanza kwa mradi, kwa kuwa una umuhimu mkubwa sana kwa taifa letu. Mradi huu utaondoa tatizo la migogoro kati ya wananchi na mwekezaji," alisema Mavunde.

Pia alisema dhamira ya serikali ni kuona wawekezaji wakubwa, wenye nia njema na Tanzania, wanapewa ushirikiano ili kuwezesha shughuli zao.

Mradi huo una thamani ya dola za Marekani milioni 125 na utatakelezwa katika vijiji vinane vilivyoko katika kata za Mikunguni, Mwera, Tungamaa na Bweni.

Mkurugenzi Mtendaji wa Nyati Mineral Sands Limited, ambaye anawakilisha hisa za serikali, Heri Gombera, alisema mradi huo unatarajiwa kuanza mwaka 2026, na unatarajiwa kuzalisha tani milioni nane za madini mbalimbali kwa mwaka.

Madini yatakayozalishwa ni Titanium, Ilmenite, Rutile, Zircon na Monazite, ambayo pamoja na matumizi mengine, hutumika kuzalisha malighafi za injini za ndege, nyuklia, vifaa vya hospitali na viwanda vya marumaru na rangi.

Alisema Nyati Minerals Sand, iko tayari kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi huo.

Uwekezaji kati ya Kampuni ya ubia ya Nyati Mineral Sands Limited na serikali ni asilimia 16, na Kampuni ya Stend Line kutoka Austaria, ina asilimia 84.

**"Nimefurahishwa na wananchi wanaoguswa na kukubali kupisha kuanza kwa mradi, kwa kuwa una umuhimu mkubwa sana kwa taifa letu. Mradi huu utaondoa tatizo la migogoro kati ya wananchi na mwekezaji," alisema Mavunde.**



Diwani wa Kata ya Terrat, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Jackson Ole Materi (wa pili kulia), akikagua mradi wa maji unaojengwa na wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), katika Kijiji cha Engonongoi juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Dawa madereva wanaofanya udanganyifu yapatikana

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MKUU wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ramadhan Ng'anzi, ametangaza kiama kwa wanaofanya udanganyifu wakati wa ukaguzi wa magari.

Amesema watu hao hasa wamiliki wa vyombo vya moto na madereva watakumbana na mkono wa dola kuanzia Machi, mwaka huu, wakati ukaguzi wa magari utakapofanyika kwa kutumia mitambo ya kidijitali.

Kamanda Ng'anzi amesema ukaguzi huo unalenga kupunguza ajali za barabarani ambazo zinaweza kuzuilika.

Ng'anzi alizungumzia ujio wa operesheni hiyo jana wakati akifungua mafunzo ya wakuu wa usalama barabarani na wakaguzi wa magari nchini yanayoendelea jijini hapa.

Alisema kwa sasa macho na masikio, haviwezi kutosha kufanya ukaguzi, hivyo uamuzi uliofikiwa ni kuanza kwa matumizi ya mitambo ya kisasa kufanya ukaguzi wa vyombo vyote vya moto.

"Mfumo wa kukagua magari kwa macho na masikio umepitwa na wakati. Hivi sasa tunakuja na ukaguzi wa mitambo ya kisasa ambayo kwa kiasi kikubwa Chuo cha Ufundi Arusha wameturahisishia kazi," alisema.

Akizungumzia mitambo hiyo, Mkuu wa Chuo cha Ufundi Arusha, Prof. Musa Chacha, alisema kutokana na utafiti uliofanywa na idara ya utafiti chuoni hapo, asilimia 70 ya ajali za barabarani nchini, zinatokana na makosa ya madereva. "Tunaamini makosa hayo ya madereva yanatokana na kukosa mafunzo ya thabiti kutoka vyuo ambavyo ni vya uhakika. Hivyo, tunafanya jitihada kuhakikisha watumiaji wa vyombo vya moto wanapata mafunzo imara ya kuwajenga na kuwaimarisha katika kazi hiyo," alisema Prof. Chacha.

Awali, Mkuu wa Idara ya Magari ya Chuo hicho, David Mtunguja, alisema mbali na kutoa mafunzo ya kuendesha magari, pia wanafundisha namna ya kuhudumia abiria.

Alisema wako madaktari ambao wanakwenda chuoni hapo kuwaelekeza madereva cha kufanya, inapotokea abiria ameugua ghafla akiwa barabarani.

"Hapa tunatoa mafunzo ya leseni za magari ya binafsi, ya abiria, ya utalii, ya kuendesha viongozi lakini hivi karibuni tutaanza kutoa leseni za kimataifa," alisema Mtunguja.

# Hospitali Marangu kuanzisha kliniki maalum umri mkubwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HOSPITALI ya Marangu (Kitemboni), iko katika hatua za mwisho za kuanzisha kliniki maalum ya magonjwa ya ndani na yale yanayoendana na umri mkubwa.

Tayari menejimenti ya hospitali hiyo, imetangaza kuwapo kwa maboresho makubwa ya uwekezaji katika kuimarisha miundombinu na vifaa tiba vya kisasa ili kuifanya kliniki hiyo kuwa na tija.

Katibu wa Afya wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Joshua Ndaga, alisema hospitali hiyo imeboresha huduma zake za tiba, uchunguzi na upasuaji.

"Jitihada za kipekee zinaendelea kufanywa sasa, chini ya kamati maalum inayoongozwa na Msaidizi wa Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, Mchungaji Deogratius Msanya, kuboresha huduma na kuzipandisha katika kiwango cha juu zaidi ili kuwaondolea adha wakazi wa maeneo yanayozunguka hospitali hiyo. "Pamoja na huduma za ngazi ya kibingwa zinazotolewa sasa, zikiwamo upasuaji wa mifupa, matatizo ya akina mama na uzazi na upasuaji mkubwa. Hospitali hiyo chini ya uongozi wa Dayosisi ya Kaskazini, umeimarisha bodi za hospitali zake, ikiwamo Hospitali ya Marangu ili kuongeza kasi ya ubora wa huduma.


"Bodi ya Hospitali ya Marangu, iko katika jitihada za kuimarisha pia eneo la rasilimali watu za hospitali ili kutoa huduma bora zaidi kwa wateja wake, wakiwa na furaha na amani ya kufanya kazi," alisema.

Hospitali hiyo iliyoko chini ya Dayosisi ya Kaskazini, inayoongozwa na Dk. Goodluck Malle, ni hospitali mlezi wa vituo vingine vilivyo chini ya Dayosisi hiyo, zikiwamo zahanati za Kiruweni, Uuwo, Mwangaria, Natiro, Uchira na Kituo cha Afya Kidia.

Hospitali hiyo ya Kitemboni, ilianzishwa na Wamisionari kutoka Leipzig- Ujerumani mwaka 1907. Wamisionari hao ni Mtawa, Elizabeth Seesemann na Sista Gesine Sammy.

Ilianzishwa kama zahanati katika eneo la Ashira hadi mwaka 1936 huduma zilipoongezwa na kupandishwa hadhi kuwa hospitali kamili.

Mwaka 1945, hospitali hiyo ilihamishwa kutoka Ashira na kupelekwa eneo la Kitemboni, ikiwa na vitanda 36 na mwaka 1989 hospitali ilikuwa na vitanda 80.





# Mikokoteni, baiskeli vyasafirisha wagonjwa kisa ubovu wa barabara

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa vijiji vya Mitonga na Ididi, Kata ya Nyamilangano, Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wanalazimika kusafirisha wagonjwa kwa kutumia baiskeli na mikokoteni kutokana na ubovu wa barabara katika maeneo hayo.

Wakazi hao wametoa kilio chao kwa nyakati tofauti na kutaja tatizo hilo kwa kukwamisha pia shughuli za kiuchumi ikiwamo usafirishaji wa mazao ya biashara kutoka kwenye vijiji hivyo.

Mkazi wa Kijiji cha Mitonga, Selina Mdewa, alisema wamekuwa wakiwasafirisha wajawazito na wagonjwa wengine kwenda hospitali ya wilaya kwa kutumia usafiri huo ambao ni hatarishi kwa afya zao na wakati mwingine kuwacheleweshea upatikanaji wa huduma.

Mkazi mwingine, Helina Manyanda, alisema mwaka juzi mdogo wake alijifungulia njiani na kuhudumiwa na watu wasio na ujuzi wowote wa kitabibu kutokana na eneo hilo kukosa miundombinu ya barabara inayoruhusu magari ya huduma kuwafikia.

"Mazao mengi, yakiwamo matunda yanaharibika kutokana na kuchelewa kufika kwenye masoko kulinganisha na mazao mengine kama pamba, alizeti, mahindi na tumbaku, hivyo tunahitaji barabara itakayomaliza tatizo na kufungua milango yetu ya kiuchumi," alisema mkazi mwingine, Shilanga Huma.

Diwani wa Nyamilangano, Robert Mihayo, alithibitisha kuwa kwa sasa uongozi wa kata hiyo, unashirikiana na Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) katika ufunguzi wa mtandao wa barabara ili kurahisisha usafirishaji.

"Barabara hiyo inajengwa kwa kiwango cha changarawe na kampuni ya M/S Arjaz Women Technology ya Shinyanga kwa kushirikiana na TARURA kwa gharama ya Sh. milioni 21.150 kuanzia Januari 22, mwaka huu tangu kutiwa saini kwa mkataba wa ujenzi huo, hivyo muda si mrefu tatizo hilo litakuwa historia," alisema Diwani Mihayo.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Kahama, Mhandisi Job Mutagwaba, alisema barabara hiyo ikikamilika ndani ya siku 120, itaondoa adha ya usafiri na usafirishaji na kwamba ujenzi huo unawanufaisha vijana wa eneo hilo ambao wanapewa ajira za muda zisizohitaji ujuzi.



Msimamizi wa Kitengo cha Wagonjwa wa dharura wa Hospitali ya Halmashauri ya Ushetu, Dk. Hisani Halihadia, akipima mzunguko wa hewa ya Oxygen mwilini kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, kwa kutumia moja ya vifaa vilivyotolewa na serikali vyenye thamani ya Sh. milioni 500, wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi(CCM) Mkoa wa Shinyanga, hospitalini hapo jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wanafunzi wenye ulemavu kujengewa bweni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Iselamagazi Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wanaotembea umbali mrefu kuifuata shule hiyo, wanatarajiwa kujengewa bweni litakalowasaidia kuondokana na adha hiyo.

Hali ya wanafunzi katika kituo hicho cha ubainishaji na upimaji wa watoto wenye ulemavu, inatajwa kuathiriwa na wanafunzi hao kutoka mbali licha ya aina mbalimbali za ulemavu walio nao, hivyo kushindwa kusoma katika mazingira rafiki.

Akieleza juzi mpango wa halmashauri kujenga bweni katika shule hiyo wakati wa hafla ya kukabidhi kiti mwendo kwa mwanafunzi Emmanuel Dotto, kilichotolewa na Shirika la Tanzania Cheshire Foundation, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Kisena Mabuba, alisema tayari bajeti imetenga, hivyo kilichobaki ni utekelezaji.

"Halmashauri tumeliona tatizo hili na tumepanga kujenga bweni kwa ajili ya watoto hawa ili wasome karibu na shule na kupata haki yao ya elimu. Baadhi wanaishi umbali mrefu kulingana na mazingira yetu huku vijijini, hivyo kusababisha wengine kukosa elimu," alisema Mabuba.

Bajeti ya ujenzi wa bweni hilo imetengwa na kupitishwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/25 unaotarajia kuanza Julai, mwaka huu na kazi hiyo inatarajia kugharimu Sh. milioni 128.

Mkurugenzi huyo alitoa wito pia kwa wazazi na walezi wilayani hapa kutowaficha watoto wenye mahitaji maalumu bali wawapeleke shuleni ili wapate haki yao ya msingi ya elimu na kutimiza ndoto zao.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Iselamagazi, Elias Litubija, alisema shule hiyo inaratibu kazi ya kuwatambua watoto wenye mahitaji maalum na kushirikiana na wazazi. Lengo la kufanya hivyo, alisema ni kuhakikisha watoto hao wanapatiwa elimu bora na kuelewa masomo na kufanya vizuri kitaaluma.

Naye mwanafunzi Dotto, alishukuru kupata msaada wa kiti mwendo huku akibainisha kuwa awali alikuwa akipata shida kwenda shuleni lakini kwa sasa usafiri huo umekuwa msaada mkubwa kwake.

# Wataka uwazi katika utekelezaji wa miradi

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WANANCHI katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, wametaka kuwapo uwazi na kutolewa taarifa za kifedha zinavyotumika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Wakizungumza juzi katika Mkutano wa Kamati ya Siasa ya Mkoa uliokuwa ukisikiliza na kutatua kero za wananchi, wananchi hao walisema hawana imani na rasilimali zinazotolewa kutekeleza miradi hiyo kama inatumika ipasavyo kutokana na kutokupata taarifa za utekelezaji.

Ntobi Athumani, mkazi wa Kijiji cha Itogwaholo, Kata ya Isaka, alisema fedha inayotolewa na mradi unaotekelezwa thamani yake ilingane na taarifa ziwekwe wazi na kuonekana sambamba na ushirikishwaji wa wananchi kwenye utekelezwaji wa miradi hiyo.

Mbunge wa Msalala, Kassim Iddi Kassim, akizungumza katika mkutano huo, alionesha kukerwa na kubadilishwa kwa mradi wa maegesho ya magari ulioibuliwa na wananchi na kuwa stendi ya mabasi ya Isaka na kukosekana kwa uwazi kwenye matumizi ya fedha za utekelezaji wake.

Alisema fedha za mradi huo zinatokana na uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (CSR) na kwamba wananchi walihitaji mradi wa maegesho ya magari kama kipaumbele chao lakini hawakushirikishwa kabla ya kubadilishwa ili watoe maoni yao.

"Mradi huu ni wa wananchi na unagharimu zaidi ya Sh. milioni 400 na walitakiwa kushirikishwa ili kujua fedha hiyo imetumikaje na kwanini matumizi yake yamebadilishwa," alisema.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Hamis Katimba, alisema uamuzi wa mabadiliko ya mradi huo yalikuwa na baraka zote za vikao na yalifanyika kupitia kikao cha kamati ya fedha uongozi na mipango.

Aliongeza kuwa uamuzi huo ulifanyika baada ya kuonekana mradi wa maegesho unaghalimu fedha nyingi, hivyo kuamua kubadili matumizi yake ili na fedha za CSR zitumika pia kutatua changamoto kwenye maeneo mengine.

Awali, ilielezwa katika kikao hicho kuwa mradi huo ulianza mwaka 2021 na unatekelezwa kwa awamu tatu kupitia fedha za CSR.

Ujenzi huo unahusisha miundombinu ya choo, kibanda cha mlinzi, ujenzi wa makalavati mawili na usawazishaji wa maeneo ya maegesho, uwekaji wa tabaka la changarawe na kushindilia molamu na kufunga taa ambao gharama yake ni zaidi ya Sh. milioni 399.

Aidha, ilielezwa kuwa miongoni mwa vitu vinavyotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa uzio wa waya ambao umeghalimu Sh. milioni 80 na jengo la abiria ambalo mpaka kukamilika kwake, litagharimu Sh. milioni 45 kutoka kwenye fedha za mapato ya ndani na ujenzi umefikia hatua ya uwezekaji.

ama

ALHAMISI FEBRUARI 22, 2024

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

## Mapinduzi ya JKCI ni makubwa, ila yanahitaji eneo zaidi la kazi



## Biashara kukusanya chupa plastiki ilivyo safisha mazingira, mkusanyaji mateso

Ukurasa 14

# Uzinduzi vipaumbele sita afya 2024/2025, Dk. Samia akianzia wagonjwa selimundu

## •Awekeza Sh. bilioni 1 kunusuru watoto 20

**Na Yasmine Protace**

WAKATI utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25 unaendelea, safari ya maendeleo inasonga katika sekta mbalimbali ikiwamo afya.

Ndani yake katika sura moja mapema mwezi huu, kumeshuhudiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akitoa fedha shilingi bilioni moja za kutibu watoto 20 wenye maradhi ya selimundu (sickle cell) nchini.

Wiki mbili baadaye, katikati ya mwezi huu, mtekelezaji na msimamizi mkuu wake katika Wizara ya Afya, Ummy Mwalimu, akatangaza vipaumbele sita vya afya kitaifa 2024/25, baadhi vikiambatana moja kwa moja na uamuzi huo wa Rais.

Hapo vinajumuisha; ubora wa huduma za afya; utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote; na mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza.

"Rais Samia amewezesha upatikanaji wa huduma bora za afya, ikiwa ni moja ya vipaumbele vya serikali yake katika kuleta maendeleo endelevu na ustawi wa jamii," anafafanua Waziri Ummy.

Imeelezwa kuwa serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, imebainisha vipaumbele sita vya kisera katika Sekta ya Afya, vitakavyoweka mkazo zaidi katika kutekelezwa kwa mwaka 2024/25, ili kuendelea kuboresha huduma za afya nchini.

Waziri Ummy Mwalimu katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kisera wa 23 wa Sekta ya Afya jijini Dodoma wiki moja iliyopita, akataja pia vipaumbele vinavyojumuisha; kuimarisha ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi kutoa huduma za afya.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipowatembelea watoto wenye selimundu, alitoa fedha za tiba kwa wanaougua maradhi hayo. **PICHA: WIZARA AFYA**

Vilevile, anataka kutolewa elimu zaidi kwa wataalamu wa afya kupatikane huduma bora; huku serikali ikitanua wigo wa huduma kiafya ngazi ya jamii.

"Serikali imejitolea kuwekeza katika mafunzo na maendeleo ya watumishi wa afya ili kuhakikisha huduma bora zinapatikana kwa wananchi," anasema.

"Ubora wa huduma za afya tunaendelea kulisisitiza kwa kuzingatia umuhimu wa kuboresha huduma kwa wateja pamoja na kuhakikisha usalama wao ili mteja apate huduma iliyokua nzuri," anasema Ummy, akisisitiza kunapatikana huduma tiba na bima afya kwa wananchi wote.

Katika hilo, Waziri Ummy, anaeleza hadi sasa muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, umeshatiwa saini na Rais Dk. Samia na Waziri Ummy anaeleza juhudi za Rais kiserikali, kwamba anahudumia jamii na kuwaimarishia huduma za afya ngazi ya jamii, pia umuhimu kushirikiana kati ya serikali na wadau wengine.

Anasema, serikali inaongeza nguvu katika mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza, kwa kutoa elimu kwa umma na kuboresha huduma za tiba.

Pia, anahimiza eneo la afya ya akili na ajali, anakosisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya serikali na sekta nyingine kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote.

### LESENI ZA MADAKTARI

Kuhusu maboresho ya leseni za madaktari, anasema serikali serikali itarejea upya na kufanyia maboresho ada za leseni za kazi kwa madaktari chini ya Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT), ikiwa sehemu ya kujibu ombi la wataaluma hao kupunguziwa gharama.

"Ada mlikuwa mkilipa kila mwaka shilingi laki moja na sasa hivi mnalipa shilingi 150,000. Kwa miaka miwili tumshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alituelekeza tupunguze angalau, imepunguza kwa kiasi.

"Dhamira ya serikali mmeiona, kwa kupunguza ada za leseni, lakini mimi na Naibu Waziri Godwin Mollel, tutaendelea kuwabana Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya na wa OR-TAMISEMI, ili tuzidi kupunguza zaidi," anasema Ummy.

Pia analitaka Baraza la Madaktari na wanachama wake kuwa na mikakati endelevu, ikiwamo ya kuwaendeleza kimasomo kufikia ngazi ya ubingwa na ubobevu, pamoja na mafunzo ya muda mfupi.

Ummy anamwelekeza Naibu wa Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, kukaa nao madaktari kuangalia makusanyo na matumizi yao, ili kuja na mpango kazi wa matumizi ya fedha hizo.

Kuhusu waganga wafawidhi kuanza kulipwa posho za madaraka, anasema Wizara ya Afya imepanga kuwalipa posho za madaraka, kutokana na kazi kubwa wanayofanya kusimamia utoaji wa huduma bora za afya, utawala pamoja na usimamizi wa miradi.

Waziri Ummy anarejea dhamira ya Rais Dk. Samia, ni kuhakikisha watumishi wanakuwa na mazingira wezeshi ya kufanya kazi, pia wanakuwa na motisha kazini.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa, anaahidi kusimamia suala hilo, ili waganga wafawidhi na vituo, waanze kupata posho za madaraka.

AFYA

# Simulizi za ndani figo inavyopandikizwa na kinachojiri kila siku katika afya jamii

Na Christina Mwakangale

COSTANTINE Lukinisha (30), amesafishwa damu au kitaalamu 'dialysis' katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH-Mloganzila), baada ya tatizo la damu kumchukua miezi minane.

Ni miongoni mwa wagonjwa wanane waliokwisha pandikizwa figo hospitalini hapo, tangu huduma ianzishwe Aprili, mwaka jana.

Costantine ni mkazi wa mkoani Mwanza, wiki hii, akiwa MNH-Mloganzila, mkoani Dar es Salaam, akirejesha tabasamu lake, baada ya kupandikizwa figo ambayo amechangiwa na mama yake mzazi mwenye umri wa miaka 51.

"Ninamshukuru Mwenyezi Mungu! Nlikuwa na changamoto ya figo nikawa nahudhuria kliniki ya 'dialysis'... kilikuwa kipindi kigumu sana, kwa kufanyiwa upandikizaji huu, kimebadilisha maisha yangu.

"Sasa najisikia vizuri baada ya kupata matibabu, natoa rai kwa wengine wenye tatizo, wafanyiwe upandikizaji na unapofanya upandikizaji unaimarika, unarejea katika majukumu yako kama awali.

"Ndugu na jamaa, waone umuhimu wa kuwachangia figo ndugu zao. Kufanya 'dialysis' ni gharama kubwa, kwa sababu unatakiwa kufanya kuanzia mara tatu kwa wiki.

"Inafanya familia kuwa katika wakati mgumu. Upendo ni kuleta furaha kwenye maisha yao na upendo wa kutoa figo, unarudisha tabasamu kama ilivyokuwa awali," anasema Costantine.

**HATUA ZA UPANDIKIZAJI**

Tabibu Bingwa wa Magonjwa ya Figo MNH-Mloganzila, Dk. Anthony Gyunda (pichani), anaielezea Nipashe kuhusu upandikizaji figo, masharti na hatua zinazotakiwa kufuatwa na mchangiaji figo.

Akiwa miongoni mwa waliomfanyia upandikizaji Costantine, hospitalini hapo, mazungumzo yake yalikuwa kama ifuatavyo:

**SWALI:** Ilichukuwa saa ngapi kufanya upandikizaji kwa Constantine?

JIBU: Mara nyingi huwa tunatumia saa nne hadi tano, kukamilisha kila kitu kuanzia kuvuna figo kutoka kwa mchangiaji na kupandikiza kwa mgonjwa.

**SWALI:** Unaposema 'kuvuna' na 'kupandikiza', ina maana kwa wakati mmoja, unafanyika upasuaji wa aina mbili, kumtoa figo mchangiaji na hapo hapo unampandikiza mgonjwa?

**JIBU:** Yeeeeees (ndio). Upandikizaji figo unahusisha upasuaji wa watu wawili kwa wakati mmoja.

SWALI: Mchangiaji anatoa figo moja tu? Na anayepandikizwa anawekewa figo moja tu? Na kwa mgonjwa figo zake ambazo zimefeli huondolewa kabisa au husogezwa pembeni tu?

**JIBU:** Ndio figo hutolewa moja kwa mchangiaji na anayepandikizwa ni moja. Hazitolewi hata zilizofeli. Huyo mgonjwa anakuwa na figo tatu (akishapandikizwa).



Mwenye nguo nyekundu, mmoja wa aliyepandikiziwa figo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.
**PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE**

**SWALI:** Anayemchangia figo ni lazima awe ndugu wa damu/kuzaliwa?

**JIBU:** Moja awe baba, mama, kaka, dada, mtoto, ndugu wa damu tu...kwa kwetu hapa Tanzania.

**SWALI:** Mchangiaji sharti ni lipi, ili achangie?

**JIBU:** Mchangiaji awe na umri usiozidi miaka 60 na usipungue 23. Afya bora na mwili na akili. Asiwe na magonjwa sugu, awe mzazi, mtoto, mwenza, ndugu wa damu kaka ama dada.

**SWALI:** Mpokeaji figo anatakiwa afuate sharti lipi?

**JIBU:** Asiwe amezidi miaka 60, afya bora na mwili na akili, awe na uwezo wa kununua dawa za kushusha kinga maisha yake yote (Immunosuppressant), atapokea figo kutoka kwa baba, mama, mwenza, mtoto, kaka ama dada.

**SWALI:** Baada ya kuchangia na kupandikiza, Je, wote watatumia dawa maisha?

**JIBU:** No! (hapana). Mchangiaji sio mgonjwa, ndio maana hata huruhusiwa ndani ya siku ya tatu, baada ya upandikizaji kwa mgonjwa. Anayebaki kutumia dawa na mgonjwa tu. Mpokeaji figo.

**HALI IKOJE?:** Tanzania, ni miongoni mwa nchi zilizo na ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza (NCDs). Takwimu za mwaka 2021 zinaonesha wagonjwa 3,440,708 walitibiwa idara ya wagonjwa wa nje (OPD) hospitali tofauti nchini.

Takwimu hizo, zinalinganishwa na 3,852,973 waliotibiwa mwaka 2022 ikiwa ni ongezeko 412,265 sawa asilimia 12.

**SHIDA YA FIGO**

Inakadiriwa asilimia 10 watu duniani kote wanasumbuliwa na magonjwa ya figo. Kila mwaka watu milioni 2.4 hufariki kutokana na magonjwa ya figo duniani kote.

Magonjwa ya figo yanashika nafasi ya sita, ni miongoni mwa magonjwa yanayochangia idadi kubwa ya vifo duniani. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

NCDs, inaongezeka kwa kasi hasa kwa nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara (SSA), huku hilo likishuhudiwa kwa ongezeko la asilimia 67 kwa kipindi cha miongo mitatu.

Takwimu za hivi karibuni za WHO, zinasema kuwa kipindi cha miaka mitano hadi 10 ijayo vifo vitokanavyo na NCDs vitaongezeka kwa asilimia 55.

Takwimu zinaonyesha kwenye kila dola moja ambayo inatolewa na kuwekezwa kwa ajili ya kinga dhidi ya magonjwa hayo, inaokoa dola saba hadi 12 kwa kila dola moja, iliyowekezwa katika kinga.

Bingwa wa Magonjwa ya Figo kutoka MNH, Dk. Onesmo Kisanga, anaeleza kwamba, wanaougua ugonjwa wa figo ni walio na umri wa kati ya miaka 18 hadi 36, umri ambao ni nguvu kazi.



Bingwa wa Magonjwa ya Figo MNH-Mloganzila, Dk. Anthony Gyunda

Dk. Kisanga, Mwenyekiti wa Chama cha Wataalamu wa Magonjwa ya Figo Tanzania (NESOT), anasema aina za magonjwa ya figo ziko mbili, ambazo ni ugonjwa wa figo wa ghafla au mshtuko (AKI) na ugonjwa sugu wa figo (CKD).

Anaeleza kuwa aina ya kwanza ambayo ni ugonjwa wa figo wa mshtuko au ghafla, ni ambao unasababisha figo kushindwa kufanya kazi yake kwa muda mfupi, kutokana na maambukizi ikiwamo malaria, kuharisha au kutapika kupita kiasi.

Pia anasema matumizi ya dawa holela mfano dawa za kutuliza maumivu zenye jamii ya 'diclofenac' pamoja na kutumia dawa za kienyeji ambazo hazijathibitishwa kitaalamu.

Anasema magonjwa ya figo ya mshtuko inaweza kutokana na mtu kupoteza damu nyingi wakati wa uzazi au ajali.

Aina ya pili, anaitaja kuwa ni ugonjwa sugu wa figo, ambao figo hudhoofika polepole na baada ya muda mrefu, uwezo wa figo hupungua kabisa na kisha figo kufeli (ESRD).

**SABABU/DALILI**

Bingwa huyo anaeleza sababu za magonjwa ya figo ni pamoja na ugonjwa wa kisukari, shinikizo la damu (HTN) pamoja na magonjwa yanayoathiri mfumo wa mkojo mfano tezi dume (BPH) na saratani.

Anasema pia uzito wa mwili uliozidi, maambukizi katika mwili ikiwamo VVU, virusi vya homa ya ini (Hepatitis B) na mtindo wa maisha ambao humfanya mtu asiwe na desturi ya kufanya mazoezi.

**GHARAMA ZAKE**

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema serikali itahakikisha huduma hiyo, inakuwa ya gharama nafuu, ili kuokoa maisha ya wengi.

"Ni sahihi kabisa gharama za kusafisha figo nchini zipo juu sana wastani wa Dola za kimarekani 100 (sawa na Sh. 250,000) kwa awamu moja.

"India ni kama Dola za Marekani 30 (sawa na Sh. 74,000) kwa siku hata hiyo dola 30 kwa siku bado ni kubwa sana, kwa Watanzania wengi ambayo ni kama Sh. 600,000 kwa mwezi, wengi hawamudu, " anasema Waziri Ummy.

Inaelezwa, hadi kufikia Machi mwaka jana, serkali kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD), ilikuwa imekamilisha ununuzi wa mashine za 'dialysis' 140 ambazo zimesambazwa kwenye vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya nchini.

Wizara ya Afya na wadau mbalimbali, ikiwamo Sirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), husisitiza umuhimu wa kufanya mazoezi.

AFYA

# Mapinduzi ya JKCI ni makubwa, ila yanahitaji eneo zaidi la kazi

**Na Dk. Felician Kilahama**

KWA historia kutoka nyenzo ya kiimani, enzi hizo, maradhi kwa binadamu hayakuwapo. Hata hivyo, kutokana na sababu mbalimbali, miili ya binadamu ikaanza kukabiliwa na changamoto za magonjwa ikiwamo maradhi ya moyo.

Nchini hadi sasa, katika kukabili maradhi hayo, kuna Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) iliyomo ndani ya Hospitali Kuu ya Taifa Muhimbili.

Taasisi hiyo ina jukumu kubwa la kupambana na maradhi ya moyo na mishipa ya damu yanayozidi kuongezeka nchini barani Afrika na sura pana ya dunia.

Uzoefu unaonyesha tangu mwaka 2016, JKCI imekuwa taasisi muhimu ya tiba kitaifa. Ikiwa ndani ya uzio wa taasisi kuu, Hospitali ya Taifa Muhimbili ambayo ina upekee wake kimatendo na kihistoria, kwamba ilizaliwa kati ya mwaka 1910 na 1920 chini ya utawala wa kikoloni, Wajerumani na Waingereza ikifahamika: Hospitali - Sewahaji.

Hata hivyo, mwaka 1956 Waingereza wakabadilisha jina kuwa "Princess Magreti Hospital". Mwaka 1961 baada ya uhuru, ikaitwa 'Hospitali ya Muhimbili' hadi mwaka 1976 ilipoitwa Muhimbili Medical Center (MMC)



Huduma zikiendelea katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete.

Mageuzi yaliendelea hadi kuifanya 'Hospitali ya Taifa Muhimbili' kupitia Tangazo la Serikali la mwaka 2000. Kupitia utaratibu huo wa Kisheria, Taasisi mbili zilizaliwa: Hospitali ya Taifa, Muhimbili na Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya Kishiriki Muhimbili (MUCHAS).

Hata hivyo, Novemba, 2004 MUCHAS ikageuzwa kuwa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS). Na Muhimbili ikabaki Hospitali Kuu ya Taifa ya Rufaa inayohudumia Watanzania na wengineo kutoka mataifa jirani wanaokuja kutibiwa nchini.

JKCI ni zao la maendeleo yaliyofikiwa, pia kufanyika tafiti kuhusu tiba asilia. Mfanikio mengine makubwa ndani ya wigo huo ni kuwapo na Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), ambayo ni chombo muhimu kinachookoa maisha ya Tanzania wengi.

Nikikumbuka tangu 2016 nilipofika JKCI mara ya kwanza na kulinganisha na hali ya sasa (2024) kuchunguza afya yangu, nashuhudia maendeleo makubwa.

Hilo ni zao la ushirikiano, ikiwamo msaada wa fedha na utaalamu kutoka serikali ya Japan. Pia, kuna ya ziada namna serikali ikajiongeza kwa mengi, kama vile kuweka sera na taratibu za kihuduma, zikiwamo za bima ya afya nchini.

Kimsingi, suala la upatikanaji huduma za afya kwa gharama nafuu na zinazotabirika na kuwa sawa nchi nzima, ni changamoto kubwa kwa wengi nchini.

Kupitia bima ya afya, inawezekana kwa wengi wakahudumiwa ipasavyo, hivyo itakuwa vyema iwapo Watanzania wengi wataelewa umuhimu wa bima ya afya kwa maisha yao; na kuchukua hatua za haraka kujiunga nazo.

Kimsingi mtu anapaswa kuchangia gharama kwa kujiunga na huduma ya bima ya afya hata kama ni mzima kwa angalizo la kesho au miaka ya mbeleni, ndio jambo linaloamsha na kuhimiza umuhimu wa watu kujiunga na bima ya afya, kuepusha changamoto kwa siku zijazo, kutokana na gharama tiba kuongezeka kila kukicha.

**JKCI ILIKOSIMAMA**

Taarifa zilizopo zinaonyesha taasisi ya JKCI ilianzishwa Septemba 5, 2015 kupitia Tangazo la Serikali la mwaka huo na hadi sana ina uwezo wa kulaza wagonjwa takribani 157 kwa wakati mmoja.

Hilo linaifanya kuwa na tafsiri ya uwezo wa kuwahudumia kila wiki wagonjwa 1800 nchini na wengine 100 kutoka nchi jirani.

Ni hatua inayoipa tafsiri, kwamba wataalamu wake wako katika heka heka za kila wakati kutibu magonjwa ya moyo, pia wakiwajibika kwenye utafiti tofauti zinazohusiana na athari za magonjwa ya moyo, huku baadhi wakipatikana madarasani MUHAS.

Mtaalamu Dk. George Longopa, bingwa anayeshughulikia maradhi ya moyo, anafafanua kuwa taasisi JKCI imejitokeza kuwa kituo muhimu cha maradhi ya moyo Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Tabibu huyo mahiri, anaongeza kuwa taasisi yao ina vitendea kazi vya kisasa, mfano anachokiita 'Cathylab, vyumba viwili vya kufanya upasuaji, chumba cha kisasa cha wagonjwa mahututi na kuwapo sehemu za wagonjwa kukaa wakisubiri huduma kutoka kwa madaktari bingwa husika.

Katika sura ya wataalamu, anasema JKCI ina watumishi wahitimu wa viwango vya juu na wanaojitoa kuwahudumia wagonjwa ipasavyo.

Hivyo anaeleza, katika kuyatimiza majukumu yake, JKCI inashirikiana na wadau kufikia malengo waliyojiwekea kitaifa, pia ya Shirika la Afya Duniani (WHO).

Dk. Longopa anaieleza taasisi hiyo imekuwa ikipokea wagonjwa kutoka nchi jirani, akitumia mfano wa Burundi, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Kenya, Malawi, Uganda, Rwanda, Somalia, Sudan, Uganda, Zambia na Zimbabwe.

**UGUMU WAKE**

Binafsi, kwa kuzingatia ninayoyaona katika kuhudumiwa hapo tangu mwaka 2016, JKCI inatoa huduma muhimu kwa wenye changamoto za magonjwa ya moyo. Hata hivyo kwa uchunguzi wa haraka, hali ya jumla inaonyesha taasisi JKCI inafanya kazi katika mazingira magumu; ikiwamo kuwa na eneo dogo sana, kulingana na majukumu yake.

**KUPANULIWA JKCI**

Miaka miwili iliyopita, nikiwa katika Hospitali ya Mloganzila, ambayo ni sehemu ya MUHAS nikashuhudia faida ya kuwa na eneo kubwa linalotosha hospitali na mahitaji yake na fursa ya maendeleo zaidi, jambo ambalo linatafsiri shauku na haja ya JKCI kuwa na nafasi kama hiyo ya maendeleo:

Hiyo ni kwa sababu, shughuli za JKCI zimepanuka sana sasa, kulinganisha na ilivyoanza, hata kufanya haja ya upanuzi wake haukwepeki.

Pili, nafasi ya kufanyia kazi na kuweka vifaa katika jengo lililopo Muhimbili, huku kukiwapo ongezeko la wahitaji wa huduma zake kutoka na ongezeko la wagonjwa wa maradhi ya moyo, hali inayofanya huduma za JKCI zihitajike maradufu.

Tatu, ni kwamba hadi sasa ni hospitali inayofanya vizuri zaidi, hata kuzua msukumo wa haja ya serikali kuangalia uwezekano wa kubadilishana sehemu iliko sasa, ikahamia penye nafasi zaidi - hospitalini Mloganzila.

Nne, pia JKCI ya leo inakabiliwa na msongamano wa wagonjwa, husani kwenye baadhi ya maeneo. Mathalani, chumba kidogo sana cha maabara; pia vyumba vidogo vya kufanya vipimo, mfano, kumchunguza mgonjwa kupitia: ECG, ECHO, kiwango cha 'stress', na kufanya 'ambulatory recording.

Tano, kimantiki sehemu ya changamoto zinazoikabili JKCI kwa kiasi kikubwa, zinasababishwa na ufinyu wa sehemu za kutoa huduma kwa wagonjwa.

Hapo ikirejewa, kongamano la siku mbili lililofanyika katika Hotel ya 'Golden Tulip' Zanzibar hivi karibuni na kuhudhuriwa na wataalamu wengi kutoka mataifa zaidi ya 30, ni ishara tosha JKCI ni chombo muhimu kitaifa na kimataifa.

Mkutano uliofunguliwa siku 12 zilizopita na Makamu wa Rais Dk. Phillip Mpango, huko Zanzibar, yanajenga ishara yatatoa mwelekeo sahihi wa manufaa ya JKCI, kuwa taasisi yenye manufaa kwa Afrika nzima.

Hapo ndipo inapoelekeza kumbukumbu kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Afya na vyombo vingine kuangalia uwezekano kwa JKCI ikipewa nafasi zaidi ya kuendesha shughuli zke zenye tija kwa umma, ikiwezekana iliko Mloganzila, hata ikaipa uwezo mkubwa wa kuhudumia magonjwa ya moyo.

Hayo yatakuwa mafanikio, kwa wakati muafaka, ikimea nje ya mipaka na Africa kwa ujumla. Nikiwa mdau mzoefu wa huduma hizo, ni hali inayoamini itaondoa uchelewеshaji usio wa lazima.

Kadhalika, uanzishaji vituo vipya katika maeneo mapya, hubeba mchakato uinachukua muda zaidi hali ambayo katika uhalisia inanchagia kusuasua huduma, maana mambo yanaingiliana.

**Sehemu kubwa ya makala hii, imeandikwa kwa uzoefu binafsi hospitalini JKCI.**




Sehemu ya majengo ya Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete.
**PICHA ZOTE: MTANDAO**

MAZINGIRA

# Biashara kukusanya chupa plastiki ilivyo safisha mazingira, mkusanyaji mateso

## • Waingiaji mtaani nao wakiri hawaaminiki

**Na Beatrice Shayo**

KUDAIWA fedha mara kwa mara zenye sura ya 'mlungula', chupa kujazwa taka kuziongezea uzito, zenye kinyesi na kupunjwa malipo mnunuzi anavyotaka, ni miongoni mwa machungu yanayowapata wanaorejeleza chupa.

Wajasiriamali hao licha ya kwamba wanasafisha mazingira kutokana na kuzagaa kwa chupa za plastiki kila kona, juhudi zao pia wanapitia changamoto lukuki.

Hapo kuna simulizi ya aliye jikoni, Shida Omary, mkazi wa Bagamoyo mkoa wa Pwani, anayejishughulisha na kununua chupa za plastiki, viroba, chuma chakavu na boksi, akisema yupo katika kazi hiyo kwa kipindi kirefu akikiri kuna changamoto lukuki.

Analifafanua kuwa jukumu linalomlipisha kodi ya Sh. 800,000 akikutana na changamoto kazini, ikiwamo kupigwa faini, akieleza kuna wakati anafuatwa ofisini na anapatiwa risiti na anakiri kuna utata kupatiwa risiti.

Omary anafafanua: "Nilishakamatwa zaidi ya mara sita, napigwa faini, iInategemea! Kuna siku wanachukua shilingi 200, 000, wakati mwingine wananipiga faini ya shilingi 300,000. Taka hizo unazoziona (anaonyesha), faini yake inakuwa tofauti mara sh 200,000 mara Sh 300,000."

Ni mazingira anayoyainisha huku mwaka 2022 katika kuzinduliwa Sera ya Taifa ya Mazingira, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango akawa na malekezo kuwa: "Sheria zetu ndogondogo kuhusiana na suala zima la hifadhi na usimamizi wa mazingira ziwekwe bayana na kusimamiwa ipasavyo, ikiwa ni pamoja na faini na adhabu mbalimbali zitakazohusika.

"Kama hizo faini ni ndogo sana, basi tuongeze, ili waharibifu wa mazingira wawajibike ipasavyo. Tuwe makini na wakali zaidi kwenye hili. Nitapenda pia kuona utaratibu wa kushindanisha mikoa na taaasisi katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira unaimarishwa."

Hapo analalamika kwamba, faini anayotozwa ni kubwa zaidi akiliinganisha na kazi anayoifanya kuisaidia serikali kuweka mazingira katika usafi, akitaja sababu ya kupigwa faini ni kukosekana ghala la kuhifadhi chupa hizo, hali inayomfanya aonekane anachafua mazingira.

"Sina uwezo wa kuzungushia ukuta. Hili eneo kwa sasa sina hizo fedha, wakiamua tu wanakuja na kunipiga faini na wananchi wanakasirika kuona haya machupa wanaona ni uchafu,"anasema Omary.



Shida Omary, mkazi wa Bagamoyo Mkoa wa Pwani, anayejishughulisha na kununua chupa za plastiki, viroba, chuma chakavu na boksi. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

Pia, anafafanua tangu kuanza biashara hiyo amekuwa akinyanyasika na kufukuzwa kila alipoifanya biashara hiyo, hata akaangukia eneo hilo, Bagamoyo, akidai yuko katika changamoto ya kuonekana msumbufu.

### MAGUMU KAZINI

Omary anafafanua magumu yake, yanajumuisha kuwekwa kinyesi na mikojo katika chupa wanazoletewa, wakitenda waokotaji kwa lengo kupata uzito zaidi.

"Tunachokifanya, tunazichambua hizo chupa na kuziweka pembeni, ili gari la taka linavyopita tunawapatia ili kupeleka dampo," anasema. Hata hivyo, Omary anaeleza mafanikio yake binafsi kuwa shughuli hiyo ya uwakala wa chupa za plastiki imemsadia kusomesha watoto na kujenga nyumba.

"Ninachokiomba serikali itusaidie isituchukulie sisi kama wahuni. Nina mchango wangu ndani ya serikali, hivyo ningeomba wasitunyanyase sisi tunaonunua hizi chupa na chuma chakavu," anafafanua Omary, akitaja baadhi ya wateja wao ni wafanyabiashara wa Kichina nchini

### ANAVYOKABILI MAGUMU

Shida anasema, kwa sasa anatamani kupata eneo kubwa la biashara hiyo, akizingatia vigezo vinavyotakiwa, ili kujiepusha na usumbufu anaoupata, ikiwamo faini za kila mara.

"Natamani kupata kiwanja ninunue hata mashine. Hapa nimeanza kidogo kidogo, nitakapokuwa vizuri, nitanunua eneo langu na baada ya hapo nitanunua mashine niwe nazisaga hizi taka," anasema Shida.

Anafafanua kuwapo kwake katika mfumo huo wa biashara taka za plastiki kuna wengi wanaomtegemea. Anatoa malelezo kuwa: "Mtu anaweza kuamka hana hela ya kula anakuja hapa ananiomba nimpatie kiroba cha kwenda kukusanya chupa, nampatia. "Anaingia mtaani na kupata ridhika sina watu rasmi yoyote anayejisikia anakuja kuleta chupa. Wengi wao tumeshazoena, anaweza mmoja anapata matatizo mtoto anaumwa namsaidia fedha ya matibabu na kuniambia nimkate atakapoleta chupa zake namsaidia haya ndio maisha yetu tunayoenda nayo,".

Omary anasema kila baada ya wiki huwa anatoa kati ya tani tatu na nne za chupa kuzipeleka sokoni. Huko nalo ana ufafanuzi wake: "Zamani ilikuwa kila siku lazima nipeleke tani mbili kwenda Dar es Salaam.

"Kwa vile tumekuwa wengi na watu wa Dar es Salaam wamekuja kufungua 'vijiwe' vyao vya kununua hizi bidhaa, nimejikuta napata nafuu ndio maana inafika wiki ndio napekeka chupa hizo kwa wachina wangu."

### BEI ILIYOKO SOKONI

Omary anayesema bei ya kilo kwa chupa sasa ni shilingi 250 na chuma kilo shiligi 650, kopo shilingi 11,000, ilhali sufuria zilizotumika kilo shilingi 3,000.

Hapo anataja bei yao kuuza kilo ya chupa shilingi 500, kilo ya chuma chakavu shilingi 500, wanauza shilinigi 900 na kilo ya aluminium soko lake linategemea kuna muda; kilo shilingi 5,000 au shilingi. 4000.

Fatuma Thabiti, wakala wa kuuza chupa za plastiki eneo la Mbagala kwa Nyoka, Dar es Salaam, anasema biashara hiyo aliianza tangu mwaka 2014 akiwa amerithishiwa na wazazi, akinena:

"Tunaowauzia hizi chupa bei kila wakati inashuka, kwa sasa sisi tunanunua shilingi 250 kutoka shilingi 350 na huko kiwandani wananunua kwetu kwa shilingi 380 kwa kilo.

"Hii ni changamoto kwetu maana hawa wanaotuletea chupa wanatulalamikia tunawaumiza wakati na sisi tunalaliwa."

Fatuma anataja shinda nyingine, ni kukosekana soko la uhakika katika kipindi kilichopo, ikiwasababishia kufanya biashara katika mazingira magumu.

Said Mohamed, ambaye ni wakala wa chupa hizo katika eneo la Yombo Mkangarawe, Dar es Salama, analalamika wanakosa pa kwenda kulalamika wanaposhushiwa bei ya chupa.

Anasema, licha ya kwa kiasi kikubwa wanaunza mazingira kupitia biashara hiyo, analalamika serikali bado haiwathamini.

"Mbali na kununua hizi chupa baadhi ya wanaotuletea hizi chupa ni 'mateja' (watumiaji dawa za kulevya). Nimejitahidi kuwabadilisha toka katika hali hiyo.

"Ninachokifanya, nazungumza nao akitaka kuacha nampeleka kituo chetu cha dini anakuwa huko siku 40, anapewa elimu akirudi mtaani amebadilika," anasema.

### WAOKOTA CHUPA

Said Mrisho, anasema wanaokota chupa kujipatia fedha za kujikimu kimaisha ingawa kinachowasumbua baadhi yao wana shida ya tabia ikiwamo wezi, jambo linalohatarisha usalama wa afya zao.

Anasema, ili kupata chupa kirahisi katika maeneo maalum, wangeandalowa maendeo mahsusi, kuzipata kuliko wanavyotembea umbali mrefu kuziokota.

Mkurugenzi wa Taasisi inayojihusisha na Utu na Mazingira (HUDEFO), Sarah Pima, anasema madhumuni yao ni kuhakikisha mazingira yanalindwa katika kudhibiti taka ngumu ikiwamo za plastiki.

Hapo anataja athari nyingi za utupaji taka ovyo na baadhi ya wananchi hawana elimu ya utunzaji taka, wengine wanatupa hadi chupa za plastiki baharini, jambo linalohatarisha uhai wa viumbe baharini, vikiwamo samaki.

Sarah anasema sheria za mazingira zipo, lakini utekelezaji wake umebaki changamoto, hata kusababisha kuzagaa kwa bidhaa hizo za plastiki mtaani, bila ya wahusika kuwajibika kuzitoa.

"Wazalishaji wa bidhaa za plastiki wanatakiwa kuwa na utaratibu wa kuhakikisha wanaziondoa bidhaa zao mitaani, baada ya kutumika ili kusaidia utunzaji wa mazingira," anasema Sarah.



## Jumuiya Wazazi CCM yabadili gia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JUMUIYA ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), imelazimika kuzibadili baadhi ya shule zake na kuzipeleka kwenye mfumo wa vyuo vya kati kutokana na kuwapo kwa ushindani mkubwa wa kupata wanafunzi.

Aidha, imewajia juu baadhi ya wanasiasa wa upinzani wanaobeza jitihada zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan hasa anaposafiri nje na ndani ya nchi kutafuta fursa za maendeleo.

Akizungumza jana kwenye kikao cha kamati ya utekelezaji ya Baraza Kuu la Jumuiya hiyo, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Taifa, Fadhili Maganya, alisema ushindani huo unatokana na uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya elimu uliofanywa na serikali kwa kuzifanya shule zake kuwa na mvuto zaidi na kuboresha utoaji wa elimu.

Mwenyekiti huyo alisema kutokana na mvuto huo imechangia jumuiya kubadili baadhi ya shule zake na kuzipeleka katika mfumo wa kuwa vyuo vya kati.

"Tuna ombi kwamba baadhi ya shule tunazibadili na kuzipeleka katika mfumo wa vyuo vya kati, tutaibua vijana wengi na tumeshakamilisha taratibu tutapeleka ombi baraza la wadhamini na vikao, shule zimejifunga kwa sababu ya ushindani lakini huko tunapokwenda tutaongeza kutoka tatu kwenda nyingine ili kusaidia wanafunzi zaidi waliomaliza kidato cha nne wakafeli hivyo kubaki mtaani," alisema.

Akitoa tamko la jumuiya hiyo kuhusu kauli zinazotolewa na baadhi ya vyama vya siasa kupitia viongozi wao za kubeza fursa anazotafuta Rais alisema safari za nje zina manufaa kwa taifa na kuifungua nchi kimaendeleo.

Alisema Rais amekuwa akihangaika huku na kule kutafuta fursa mbalimbali ambazo kila Mtanzania ni shahidi wa hilo kwa kuwa zimekuwa na manufaa .

"Hivi karibuni kumejitokeza watu wakibeza hasa Rais anaposafiri ndani na nje ya nchi kutafuta misaada, nitumie fursa hii kuwaasa wote wanaobeza jitihada anazofanya Rais, nawasihi wamwache nchi ya Tanzania ifunguke kiuchumi.

"Nchi hii si iliyoendelea bali inaendelea, ni kweli tuna uhuru lakini hatuwezi kupiga hatua haraka tunaenda taratibu, mwenda bure si sawa na mkaa bure huenda akaokota, mgaa gaa na upwa hali wali mkavu pia mguu mtembezi usiporudi na umande utarudi na mwiba," alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Dogo Iddi Mabrouk, alisema jumuiya hiyo ni kubwa haina ubaguzi inachukua watu wa rika zote hivyo itandelea kusimamia suala la maadili.

Kanali Mstaafu Iddi Kipingu ambaye amepewa jukumu la kufanya mapitio ya shule hizo, alisema kumekuwa na dhana potofu kuwa shule bora ni ile inayofaulisha sana na kuwataka kuondokana na tafsiri hiyo kwa kuwa shule nzuri ni ile inayotafsiri matatizo ya watoto.

# Takwimu afya ya akili zaibua mapya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAKWIMU za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha nusu ya magonjwa ya akili duniani yanaanza katika umri wa miaka 14 huku vyanzo vikuu vikitajwa kuwa msongo wa mawazo na matumizi mabaya ya pombe na mihadarati.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe imejipanga kuanzisha mafunzo mbalimbali kwa wauguzi wa afya ya akili ngazi ya stashahada ikiwa ni mikakati ya kuondokana na tatizo hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Paul Lawala, alisema kwa sasa timu ya watalaamu iko mkoani Iringa ili kuandaa uanzishwaji wa mafunzo hayo.

"Kozi zingine ambazo zinapaswa kuwepo na kutengenezewa mitaala ni kozi ya maofisa ustawi wa jamii wa afya ya akili na kozi za tiba kwa ngazi ya stashahada na shahada ya kwanza," alisema.

Naye Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, alisema wamejipanga kuangalia namna ya kuwa na eneo la kuwaweka wagonjwa kabla ya kuwapeleka kwenye Hospitali ya Mirembe.

Nao baadhi ya wananchi waliomba serikali kupeleka wataalamu vijijini ili kutoa elimu namna ya kukabiliana na tatizo hilo hasa kwa vijana.

Mkazi wa Dodoma, Kuluthumu Ibrahim, alisema wataalamu wa saikolojia wanapaswa kuwezeshwa kuifikia jamii kutoa elimu ya kukabiliana na tatizo hilo.



Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, wakiangalia utunzaji wa mazingira walipofanya ziara ya kikazi katika mgodi wa Barrick North Mara, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jafo ataja mafanikio katazo kuni, mkaa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ameeleza namna taasisi zinazolisha zaidi ya watu 100 kwa siku zilivyookoa gharama za uendeshaji zilizokuwa zinatumika kununua kuni na mkaa.

Miongoni mwa taasisi hizo ni Shule ya Sekondari Ruvu mkoani Pwani ambayo ilikuwa ikitumia Sh. milioni sita kwa mwezi lakini kwa sasa inatumia nishati safi ya gesi kwa gharama ya Sh. milioni mbili kwa muda huo.

Akizungumza na Nipashe jana ikiwa ni siku moja baada ya kueleza utekelezaji wa katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa taasisi lililotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan Novemba mosi, 2022 Dk. Jafo alisema serikali itaendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa taasisi zake ili zifikie lengo la kuachana kabisa na matumizi ya kuni na mkaa. Alisisitiza kuwa katazo hilo haliwahusu wananchi ngazi ya kaya.

"Kila mwaka wa bajeti huwa tunatenga fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo ambayo huwa inaenda kwenye matumizi ya kuni na mkaa. Sasa inaonyesha wazi waliongia kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia wamepunguza kwa kiasi kikubwa matumizi ya fedha za serikali."

"Nitoe mfano Shule ya Sekondari ya Ruvu ambayo mwanzo walikuwa wanatumia wastani wa Sh. milioni sita kwa mwezi kwa hiyo ukipiga kwa miezi 12 utaona kwa namna gani wanatumia fedha kwa mwaka mmoja. Baada ya kufunga mtungi wamepunguza na kutumia Sh. milioni 24 kwa mwaka badala ya Sh. milioni 72. Kwa hiyo kwa haraka unaona wameweza kuokoa Sh. milioni nne kwa mwezi kwa hiyo unaona hii ni faida kubwa sana," alisema.

Dk. Jafo alisema sekta ya elimu kupitia taasisi zake zikiwamo shule ambazo zimetekeleza agizo hilo kwa asilimia 85, zimeokoa miti ambayo ingekatwa kwa ajili ya nishati ya kupikia.

"Tunatoa hamasa kwa taasisi zote kuendelea kutekeleza agizo la serikali la kutumia nishati safi ya kupikia kwa kuwa zile taasisi zilizoanza kutumia nishati hiyo, zimeanza kupata faida. Lakini pia matumizi ya kuni husababisha madhara katika mfumo wa upumuaji," alisema.

Waziri Jafo aliongeza kuwa matumizi ya kuni na mkaa huchangia ukataji wa miti na kusababisha uharibifu wa mazingira ambayo huleta ukame kutokana na kutokunyesha kwa mvua.

Alisema zaidi ya hekta 462,000 kila mwaka zinapotea kutokana na vitendo vya ukataji wa miti na kusababisha uhaba wa mvua ambao huchangia kutokujaa kwa mabwawa ya kufua umeme na ndio chanzo cha mgao wa umeme.

Dk. Jafo pia alisema kuwa ukame huathiri kilimo kwa kuwa asilimia kubwa ya sekta hiyo hiyo hutegemea mvua hivyo wananchi wanahimizwa kupanda miti badala ya kuikata.

Hata hivyo, alisema mradi wa bwawa la kufua umeme la Mwalimu Julius Nyerere unahitaji mvua za kutosha hivyo wananchi wana kila sababu ya kushiriki kikamilifu katika kutunza misitu iliyopo.

Aliwapongeza mabalozi wa mazingira kwa kujitoa kwao katika kuhamasisha jamii kuhusu masuala ya utunzaji wa mazingira kwenye maeneo mbalimbali nchini.





# Mwabukusi afufua upya sakata bandari

Na Nebart Msokwa, MBEYA

SAKATA la uwekezaji wa bandari ya Dar es Salaam limeibuka upya baada ya Wakili Bonface Mwabukusi kutangaza kulipeleka katika Mahakama ya Rufani akisisitiza kuwa yeye watahakikisha rasilimali hiyo ya taifa inabaki kuwa ya Watanzania.

Mwabukusi alitangaza kufufua upya kesi hiyo juzi kwenye mkutano wa hadhara wa viongozi wa kitaifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wananchi uliofanyika katika Uwanja wa Ruanda Nzovwe jijini Mbeya.

Alisema awali walikwenda kufungua kesi katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya kwa lengo la kupinga uwekezaji huo na wakashindwa.

Alisema baada ya kushindwa waliwaahidi Watanzania kuwa watakata rufani kwenye mahakama ya rufani jambo ambalo wanakusudia kulitekeleza hivi karibuni.

"Kuna watu wanajidanganya kwamba suala la bandari limekwisha, sisi tulishasema na tunarudia tena bandari ni urithi wetu hatutakubali iuzwe, tunakwenda kwenye mahakama ya rufani ili kuhakikisha bandari yetu inakuwa salama," alisema Mwabukusi. Alisema yeye pamoja na Watanzania wengine ambao wako kwenye kundi la 'Sauti ya Watanzania' watahakikisha wanapambania rasilimali zote za taifa ili ziendelee kuwanufaisha wananchi wa Tanzania.

Hata hivyo, Mwabukusu aliililaumu Bunge la Tanzania kwa kubariki uwekezaji wa bandari hiyo akidai kuwa haliwasaidii wananchi wa Tanzania.

Mwaka jana, Mwabukusi na wenzake walifungua kesi mahakamani ya kupinga Mkataba wa Uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam kati ya Serikali na kampuni ya DP World ya Dubai.



Mjumbe wa Jumuiya ya Amani na Maridhiano Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Elica Mwakyolile, akipanda mti nje ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwa niaba ya viongozi wanawake wa jumuiya hiyo, wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Amani na Maridhiano hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Faini 50,000/- uchimbaji holela mchanga

Na Elizabeth John, NJOMBE

WATU watakaobainika kuchimba mchanga na kufyatua matofali bila kibali na kusababisha madimbwi katika maeneo yenye makazi ya watu katika halmashauri ya mji wa makambako kutozwa faini ya Sh. 50,000.

Taarifa hiyo ya hadhari imetolewa ikiwa ni siku chache baada ya mtoto Cosmas Gadau (13), mkazi wa Mtaa wa Igangidung'u kufariki dunia Febuari 17, mwaka huu, baada ya kuingia kwenye dimbwi la maji wakati akitoa tairi alilokuwa anachezea.

Mtendaji wa Serikali ya Mtaa wa Igangidung'u, Happiness Sanga, alisema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wakati wa kufukia madimbwi yaliyosababishwa na shughuli za uchimbaji mchanga na ufyatuaji wa matofali.

"Atakayekutwa anaendeleza shughuli za uchimbaji pale atahesabiwa kuwa ni muuaji kama wauaji wengine kwa sababu unatengeneza chanzo cha ajali. Shughuli za matofali huwezi kufanya mpaka upate kibali na kibali chenyewe kuchukulia mpaka halmashauri kwa sababu mashimo mengine ni makubwa," alisema Sanga.

Awali, wananchi wa mtaa huo waliiomba serikali kuwachukulia hatua za kisheria wananchi wote ambao wanafyatua matofali na kuchimba mchanga ya ujenzi kwenye makazi ya watu. Walisema uchimbaji huo holela umekuwa ukisababisha madhara kwa watoto.

Maria Mhagama alisema ili kukabiliana na tatizo hilo ni lazima serikali iwachukulie hatua za kisheria watu wote wanaojihusisha na uchimbaji wa mchanga wa ujenzi na ufyatuaji matofali ambao umesababisha uwapo wa madimbwi mengi na kuhatarisha usalama wa watoto.

"Tumepita katika sehemu zote ambazo walikuwa wakichimba mchanga tumefukia madimbwi yote, lakini tunaomba serikali iwachukulie hatua kali watu ambao watachimba tena mchanga na kufyatua tofali kwenye makazi yetu," alisema Mhagama.

Naye Antony Gadau alisema ni vyema serikali ikawazuia wanaochimba mchanga katika makazi ya watu kwa sababu ni hatari kwa usalama wa watoto na watu wazima majira ya usiku.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Igangidung'u, Emmanuel Gadau, aliwataka wananchi wa mtaa huo kuendelea kufukia madimbwi mengine yaliyopo katika mtaa huo, huku akiwataka kuzingatia utaratibu na sheria walizojiwekea za kutunza mazingira.

Mtendaji wa Kata ya Kivavi, Daria Kilasi, aliwataka watendaji wa mitaa kusimamia sheria ndogo katika mitaa yao ili kuhakikisha usalama wa raia na mali zao.

"Niwatake wananchi wafuate sheria, wasisubiri tuwapige faini alafu wailaumu serikali kwamba inawaumiza wafuate sheria, wafuate vibali waweze kufanya kila kitu kwa utaratibu uliyowekwa," alisema Kilasi.

# Mvua yakata mawasiliano

Na Nebart Msokwa, MBEYA

MVUA inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali mkoani Mbeya, imesababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara za vijijini.

Pia imesababisha mawasiliano kukatika kwenye baadhi ya maeneo na kukwamisha shughuli za kiuchumi ikiwamo kilimo na baadhi ya maeneo wakulima wanashindwa kusafirisha pembejeo za kilimo kwenda mashambani na kusafirisha mazao kutoka shambani kwenda sokoni.

Hayo yaliibuliwa na wawakilishi wa wananchi kwenye kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Mbeya kilicholenga kujadili utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara mkoani hapa.

Mbunge wa Mbarali, Bahati Ndingo, alisema barabara zote za pembezoni katika jimbo hilo hazipitiki, hivyo akaomba Wakala wa Barabara za Mjijini na Vijijini (TARURA) kuangalia uwezekano wa haraka wa kutengeneza barabara ambazo ni muhimu kwa wananchi.

Ndingo alisema asilimia kubwa ya wananchi wa Mbarali wanategemea shughuli za kiuchumi ambazo msingi wake mkuu ni uwepo wa miundombinu bora ya barabara kwa ajili ya kusafirisha mazao yao na pembejeo za kilimo.

"Mheshimiwa Mwenyekiti ni ukweli usiopingika kwamba baada ya mvua kunyesha hali ya barabara maeneo yetu ya vijijini ni mbaya sana na sisi kule Mbarali ni wakulima, sasa hivi hata ile tija ya mbolea za ruzuku ambayo Serikali imetupa inakuwa ndogo kwa sababu mkulima anashindwa kusafiri kufuata mbolea hiyo,"alisema Ndingo.

Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njenza, alisema baadhi ya barabara katika jimbo lake zimekatika kabisa, hivyo wananchi wanashindwa kusafiri kutoka eneo moja kwenda linguine.

Njenza alizitaja barabara hizo kuwa ni pamoja na barabara ya Ilambo- Somanga, Nyalwela- Mbonile, Ilembo –Isonso na Mbalizi-Shigamba ambayo alidai imekuwapo kwenye bajeti muda mrefu lakini utekelezaji wake unasuasua.

"Hali ya barabara zetu ni mbaya mno hali ambayo imeleta kero kwa wananchi wetu kwa sababu inakwamisha shughuli zao, tunaogopa hata kwenda kuwasikiliza maana wana hasira sana, wamechoka na majibu tunayowapa, niombe utekelezaji wa hili," alisema Njenza.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Alberto Kindole, alikiri miundombinu mingi ya barabara za vijijini mkoani humo kuharibika kipindi cha mvua na kwamba kinachokwamisha matengenezo ni ufinyu wa bajeti.

Alisema fedha ambazo huwa wanapelekewa kila mwaka huwa zinakuwa hazitoshelezi mahitaji ya ukarabati wa barabara zilizoko ndani ya mkoa huo akidai kuwa wana mtandao mrefu wa barabara.

"Mwaka jana tuliletewa Sh. bilioni nane kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 156 lakini mpaka mwezi Disemba mwakajana tulipokea Sh. Milioni 900 pekee, kwa sasa tunaendelea kuwasiliana na makao makuu ili watuongezee fedha," alisema Kindole.

Aliwaomba wadau mbalimbali wakiwemo wakandarasi kuendelea kujibana kwa fedha zilizopo ili baadhi ya miundombinu itengenezwe.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliagiza TARURA kuhakikisha wanarejesha mawasiliano kwenye maeneo ambayo barabara hazipitiki kabisa ili kunusuru maisha ya wananchi.

Vilevile aliwataka kutumia mapato yao ya ndani kufanya ukarabati wa baadhi ya miundombinu hiyo wakati wanaendelea na mawasiliano na makao makuu.



## HABARI ZANZIBAR

## Faida za Tanzania kidijitali zatajwa

**Na Rahma Suleiman** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mohammed Khamis Abdulla, amesema utekelezaji wa mradi wa Tanzania ya Kidijitali utawezesha upatikanaji wa huduma bora za mawasiliano na kuchochea matumizi ya teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA).

Aliyasema hayo jana visiwani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa mradi huo wa miaka mitano ulioanza mwaka 2021 unaogharimu Dola za Kimarekani milioni 150 ambazo ni mkopo wa fedha kutoka Benki ya Dunia.

Abdulla alisema mradi huo utarahisisha utekelezaji wa mkakati wa kukuza uchumi wa kidijitali katika zama hizi za mapinduzi ya viwanda ambazo matumizi ya TEHAMA ni nyenzo muhimu katika ustawi wa uchumi na maendeleo ya taifa.

Katibu Mkuu huyo alisema katika kuchochea mabadiliko ya kidigitali nchini, mifumo mbalimbali inatengenezwa ambayo itawezesha upatikanaji wa huduma bora na kwa wakati na baadhi ya mifumo hiyo.

Alitaja mifumo hiyo ni uundwaji wa mfumo wa namba ya utambulisho na jamii namba ambayo itatumika kufanya utambuzi kuanzia mtu anapozaliwa, hivyo kumwezesha mwananchi kupata huduma zikiwamo afya, elimu na usafiri.

“Mfumo huu utaunganishwa na mfumo wa NIDA (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa), RITA (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini), ZCSRA, Anuani za Makazi na mfumo wa Idara ya Uhamiaji Pamoja na mfumo wa Kitaifa wa Uunganishwaji wa Mifumo utakaounganisha mifumo ya serikali na binafsi ili kuwezesha utoaji wa huduma kwa wananchi,” alisema.

Katibu Mkuu pia alisema lengo lingine kuendelea kuboresha mfumo wa anwani za makaazi na postikodi kwa lengo la kuwezesha watoa huduma kutambua wateja wao kielektroniki ili kuondoa adha ya mwananchi ya kwenda kila mara kuomba utambulisho kwenye serikali za mitaa.

Aliyataja malengo mingine ya mradi kuwa ni kuwezesha kupeleka mawasiliano ya mtandao wa simu maeneo ambayo hayakuwa na mawasiliano na kwamba kwa sasa serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, inaendelea na ujenzi wa minara mipya 438 ya simu na upandishaji hadhi minara 304 kwenye maeneo ya vijijini na pembezoni mwa Tanzania yasiyo na mvuto wa kibiashara.

“Mradi huu utawezesha kuunganisha taasisi za serikali 891 na Mtandao wa Mawasiliano ya Serikali (GovNet) ili kufikisha mawasiliano ya kimtandao kwenye ofisi hizo zinazojumuisha hospitali, vituo vya afya, shule, mahakama, vituo vya polisi, halmashauri na taasisi za serikali,” alisema.

Naye Katibu Mkuu Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Khadija Mbarouk, aliwataka Wazanzibari kuchangamkia fursa za ufadhili wa masomo kupitia mradi huo ambao lengo lake ni kunufaisha pande zote mbili za Muungano.

Alisema mafunzo hayo yatawezesha kuwa na watalamu wengi watakaoweza kuvitumia vituo vya ubinifu vya TEHAMA kwa ajili ya kupata maendeleo.

# Visiwa hatarini kisa mabadiliko tabianchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VISIWA vingi vidogo viko hatarini kutoweka kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kutokana na ongezeko la maji baharini linalotokana na mabadililo ya tabia nchini, imeelezwa.

Aidha, ripoti za kitaalam zinaonyesha kuwa hadi sasa maeneo 20 yakiwamo tisa Unguja na 11 Pemba, yameathirika kwa kuingiwa na maji ya bahari kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Maeneo hayo yamebainika baada ya kufanyika utafiti mdogo uliofanywa na Idara ya Maendelea ya Kimataifa (DFID) kutoka Uingereza mwaka 2012. Utafiti huo uliangalia athari za mabadiliko ya tabianchi kwa uchumi wa Zanzibar.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mtambwe, Mohammed Ali Suleiman.

Katika swali hilo, Suleiman alitaka kujua kama serikali imewahi kufanya tathmini ya kina ya kitaalamu kuhusu athari hizo kwa visiwa hivyo kwa upande wa mazingira, kijamii, na kiuchumi.

Waziri Suleiman alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi, ripoti za kitaalamu zinaonyesha kuwa visiwa vingi viko hatarini kutoweka kutokana na ongezeko la kiwango cha maji baharini.

Alisema serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilifanya utafiti mdogo wa maeneo maeneo 20 ambayo yaliathirika kwa kuingiwa na maji ya Bahari nas kwamba utafiti huo ulikusanya taarifa za kina za maeneo hayo zikiwamo ukubwa wa athari, shughuli zinazofanyika katika maeneo hayo na kupendekeza njia mbalimbali za kuyarejesha katika uhalisia ili yaendelee kutumika kwa kilimo na shughuli zingine za kijamii.

“Mheshimiwa Spika, kwa kuwa si rahisi kuepuka athari za mabadiliko ya tabianchi, serikali imeamua kuweka mikakati endelevu ili kudhibiti kasi ya athari zinazoweza kujitokeza katika maeneo mbalimbali,” alisema.

Alitaja mikakati hiyo kuwa ni pamoja na kufanya mapitio ya Mkakati wa Zanzibar wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2014 na kuendelea kutekeleza miradi ambayo itasadia wananchi wa maeneo yaliyoathirika kujikimu kimaisha kwa kujenga ukuta na matuta kuzuia kupitisha maji ya chumvi.

Pia alisema kazi nyingine ni kuandaa mpango wa kuirithisha Zanzibar ya Kijani (green legacy programe) kwa kupanda miti na kuitunza katika maeneo yote yanayohitaji kurejeshwa uhasilia wake yakiwamo maeneo ya fukwe na pembezoni mwa bahari.

“Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeshirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kuandaa ripoti ya kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (Climate Adaptation Country Compacts, 2023) ambayo inatoa taswira nzima za hatua na makisio ya fedha zinazohitajika katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania,” alisema.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Salum Mkuya akizungumza katika kikao cha Baraza la wawakilishi, Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mradi vyoo kunufaisha wanafunzi 2,050

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

ZAIDI ya wanafunzi 2,050 kutoka Shule ya Msingi Kisiwandui, Unguja, wanatarajia kunufaika na mradi wa ujenzi wa matundu ya vyoo na maboresho ya vifaa vingine.

Shule hiyo ina idadi ya wanafunzi kuanzia elimu ya maandalizi hadi msingi, wakiwamo wenye ulemavu na mahitaji maalum lakini ina matundu 10 pekee ya choo.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa mradi huo unaotekelezwa na Kampuni ya Puma Energy Tanzania, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa, alisema kujengwa kwa vyoo hivyo kutasaidia kuongeza mahudhurio ya wanafunzi shuleni hapo.

Alisema mradi huo pia utasaidia katika kuunga mkono juhudi za serikali kupunguza uhaba wa matundu ya vyoo kwa wanafunzi shuleni.

“Nimefurahi kuona juhudi za Puma Energy katika kujizatiti kuboresha mazingira mazuri ya kujifunzia shuleni. Nimefahamishwa kuwa jitihada hizi haziishii shuleni hapa Kisiwandui bali mradi utaendelea kutekelezwa katika shule tofauti visiwani Zanzibar,” alisema Lela.

Meneja Mkuu wa Puma Energy Tanzania, Fatma Abdullah, alisema wataendelea kujitolea katika kuleta maendeleo chanya kwa jamii inayoihudumia.

Alisema katika kuboresha upatikanaji wa maji safi, vifaa vya usafi wa mazingira katika Shule ya Msingi Kisiwandui wamechangia Sh. milioni 130.

“Puma Energy imeanzisha mradi uitwao ‘Energizing School Communities’ (kuzipatia nguvu shule za umma) ili kuunga mkono elimu na kuhamasisha mazingira yenye afya ya kujifunzia na kuboresha matokeo bora ya elimu kwa wanafunzi wa Tanzania,” alisema.

“Wanafunzi wa Kisiwandui wanakuwa wa kwanza kunufaika na mradi huu ambapo wamesaidiwa kuboreshewa idadi ya matundu ya choo,” alibainisha.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Taifa ya Shule ya WASH (2018), asilimia 25 ya shule za Tanzania zimefikia viwango vya kawaida vya serikali vya matundu ya choo kwa wanafunzi na asilimia 16.7 ya shule hutoa vyumba vya kubadilishia vyenye mahitaji ya msingi kama vile maji, mapipa ya taka, sabuni, na vifaa vya dharura.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**LUCY M. JULIUS** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye **Index No. S1062 - 0040** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MALENGA SECONDARY SCHOOL mwaka 2013.** Cheti cha chuo, ASTASHAHADA YA UHANDISI WA MAJI chenye No. **OD/2016/WS276.** kilichotolewa na **CHUO CHA MAJI DAR ES SALAAM** mwaka 2020, pamoja na cheti cha kuzaliwa. vyeti hivi vimepotea kisasa - Dodoma. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/4543/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ERICK FARES TARIMO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1522-0055** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SCOLASTICA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/23476/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**OMARI HIZZA MBWANA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA "PASSPORT" ILIYOTOLEWA NA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA YENYE USAJILI **TAE 0419210** ,YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/1989/2024.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 27477 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late YESAYA YOEZA MGONJA DECEASED OF MIYUJI STREET, DODOMA CITY COUNCIL**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY ANNA YESAYA MGONJA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. No.369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 06 Day of 03, 2024
Dated at Dodoma this 21 Day of 02, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LAWRENCE ERNEST NATHAN** anatangaza lupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CLUGER** yenye usajili namba **T578 BTQ,** CHASSIS NAMBA: **ACU250028201** na ENGINE NAMBA: **2AZ1330287.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/NJO/NJO/277/2024**

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**LAND CASE NO. 26059 OF 2023**

**PENUEL HILDA LAISER..........................PLAINNTIFF**

**VERSUS**

**TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED & OTHERS...DEFENDANTS**

**TO;**
**DEONATUS JULIUS,**
**P.O.BOX 34634 ,**
**DAR ES SALAAM.**

**NOTICE OF DATE FOR MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for **MENTION 26TH FEBRUARY, 2024** at 10:00AM Before **HON. S. MWAIPOPO, JUDGE.**
**YOU ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail.
**GIVEN UNDER MY Hand** and seal of the court this 12TH day of FEBRUARY, 2024.

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**LAND CASE NO. 26059 OF 2023**

**PENUEL HILDA LAISER........................PLAINNTIFF**

**VERSUS**

**TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED & OTHERS.........DEFENDANTS**

**TO;**
**IBRAHIM MICHAEL HAPE,**
**P.O.BOX 34634 ,**
**DAR ES SALAAM.**

**NOTICE OF DATE FOR MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for **MENTION 26TH FEBRUARY, 2024 at 10:00AM** Before ***HON. S. MWAIPOPO, JUDGE.***
**YOU ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail.
**GIVEN UNDER MY Hand** and seal of the court this 12TH day of FEBRUARY, 2024.

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**LAND CASE NO. 26059 OF 2023**

**PENUEL HILDA LAISER........................PLAINNTIFF**

**VERSUS**

**TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED & OTHERS......DEFENDANTS**

**TO;**
**ALLAN NALIGIA MAGOMA,**
**P.O.BOX 9373 ,**
**DAR ES SALAAM.**

**NOTICE OF DATE FOR MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for **MENTION 26TH FEBRUARY, 2024** at 10:00AM Before **HON. S. MWAIPOPO, JUDGE.**
**YOU ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail.
**GIVEN UNDER MY** Hand and seal of the court this **12TH day of FEBRUARY, 2024.**

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**LAND CASE NO. 26059 OF 2023**

**PENUEL HILDA LAISER..........................PLAINNTIFF**

**VERSUS**

**TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED & OTHERS.........DEFENDANTS**

**TO;**
**MAZIKU BUNDALA,**
**P.O.BOX 34634,**
**DAR ES SALAAM.**

**NOTICE OF DATE FOR MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for **MENTION 26TH FEBRUARY, 2024 at** 10:00AM Before **HON. S. MWAIPOPO, JUDGE.**
**YOU ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail.
**GIVEN UNDER MY** Hand and seal of the court this 12TH day of FEBRUARY, 2024.

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**LAND CASE NO. 26059 OF 2023**

**PENUEL HILDA LAISER...............PLAINNTIFF**

**VERSUS**

**TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED & OTHERS.........DEFENDANTS**

**TO;**
**THE MANAGING DIRECTOR,**
**FJS AFRICAN STARCH DEVELOPMENT COMPANY LIMITED**
**P.O.BOX 34634,**
**DAR ES SALAAM.**

**NOTICE OF DATE FOR MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for **MENTION 26TH FEBRUARY, 2024 at 10:00AM** Before **HON. S. MWAIPOPO, JUDGE.**
**YOU ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail.
**GIVEN UNDER MY Hand** and seal of the court this 12TH day of FEBRUARY, 2024.

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**LAND CASE NO. 26059 OF 2023**

**PENUEL HILDA LAISER........................PLAINNTIFF**

**VERSUS**

**TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED & OTHERS......DEFENDANTS**

**TO;**
**RONALD SYLVESTER RWEGASIRA,**
**P.O.BOX 34634,**
**DAR ES SALAAM.**

**NOTICE OF DATE FOR MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for **MENTION 26TH FEBRUARY, 2024 at 10:00AM** Before **HON. S. MWAIPOPO, JUDGE.**
**YOU ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail.
**GIVEN UNDER MY Hand** and seal of the court this 12TH day of **FEBRUARY, 2024.**

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**LAND CASE NO. 26059 OF 2023**

**PENUEL HILDA LAISER..........................PLAINNTIFF**

**VERSUS**

**TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED & OTHERS...........DEFENDANTS**

**TO;**
**EDWIN PANCRAS KATO,**
**P.O.BOX 34634,**
**DAR ES SALAAM.**

**NOTICE OF DATE FOR MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for **MENTION 26TH FEBRUARY, 2024 at 10:00AM** Before **HON. S. MWAIPOPO, JUDGE.**
**YOU ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail.
**GIVEN UNDER MY** Hand and seal of the court this 12TH day of FEBRUARY, 2024.

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**LAND CASE NO. 26059 OF 2023**

**PENUEL HILDA LAISER........................PLAINNTIFF**

**VERSUS**

**TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED & OTHERS........DEFENDANTS**

**TO;**
**MARWA MTALAI,**
**P.O.BOX 34634,**
**DAR ES SALAAM.**

**NOTICE OF DATE FOR MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for **MENTION 26TH FEBRUARY, 2024** at 10:00AM Before **HON. S. MWAIPOPO, JUDGE.**
**YOU ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail.
**GIVEN UNDER MY Hand** and seal of the court this **12TH day of FEBRUARY, 2024.**

DEPUTY REGISTRAR

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA. 364 YA MWAKA 2013**

**ALICE MHOJA ABEL ....................................... MDAI**

**DHIDI YA**

**PAULO JUMA ............................................... MDAIWA**

**KWA:**
**PAULO JUMA**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 28.03.2024 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 21 ya mwezi wa FEBRUARI, 2024

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 3254 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE SAULI JEREMIA MWAKISUNGA**

**AND**

**In the matter of Application for letters of administration by:-**
**SYONI SAULI MWAIKAMBO..................PETITIONER**

**GENERAL CITATION (Rule 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 20th day of March 2024.

Dated at Kyela, this 20th day of February, 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE I/C
KYELA.

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,
KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Afrika Kusini kufanya uchaguzi Mei 29

**CAPETOWN,** AFRIKA KUSINI

UCHAGUZI mkuu wa majimbo Afrika Kusini umepangwa Mei 29, ukienda sambamba na maadhimisho ya miaka 30 ya uhuru.

Kulingana na ofisi ya rais, hatua hiyo imeafikiwa baada ya kiongozi wa nchi hiyo, Rais Cyril Ramaphosa, kushauriana na tume ya uchaguzi kuhusu tarehe ya uchaguzi huo.

Hata hivyo, Rais Ramaphosa aliitisha kikao cha dharura na wakuu wote wa mikoa na tume kujadili matayarisho ya uchaguzi huo.

Wapigakura wanatarajiwa kuwachagua wabunge wa kitaifa pamoja na wa mikoa katika kila jimbo kati ya majimbo tisa yanayounda nchi hiyo.

Kiongozi huyo anawania kuongoza kwa muhula wa pili.

Chama chake cha African National Congress (ANC) kinakabiliwa na ushindani mkali katika uchaguzi huo, huku kura za maoni zikionyesha kuwa kinaweza kupoteza umaarufu wake kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 30.

Afrika Kusini ilifanya uchaguzi wake wa kwanza wa kidemokrasia mwaka 1994 kufuatia kumalizika kwa mfumo wa ubaguzi wa rangi, wakati hayati Nelson Mandela alipochaguliwa kuwa rais. **RFI**

## Uingereza yashindwa kurusha kombora hatari

**LONDON,** UINGEREZA

UINGEREZA imeshindwa jaribio lake la kurusha kombora la Trident kutoka kwenye nyambizi ya kijeshi ya Royal Navy.

Jaribio hilo lilifanywa katika nyambizi ya HMS Vanguard karibu na pwani ya mashariki ya nchi ya Marekani.

Kulingana na gazeti la The Sun, roketi za kuongeza nguvu kombora hilo zilishindwa kufanya kazi na kusababisha kutua baharini karibu na eneo hilo.

Makombora ya aina hiyo pia inatazamiwa kubeba vichwa vya nyuklia.

Kutokana na kushindwa kwa jaribio hilo, imeelezwa ni kwa Uingereza na Marekani ambao hutengeneza makombora ya Trident.

Waziri wa Ulinzi Grant Shapps na mkuu wa Jeshi la Wanamaji walikuwa kwenye meli ya HMS Vanguard, kushuhudia tukio hilo mwezi wa Januari.

Kama jaribio hilo lingefanikiwa, makombora hayo yalitakiwa kuruka maili elfu kadhaa kabla ya kutua bila madhara katika bahari ya Atlantiki kati ya Brazil na Afrika Magharibi. Badala yake kombora hilo lilidondoka ndani ya bahari karibu na liliporushwa.

# Waziri Mkuu DRC ajiuzulu

**KINSHASA,** DRC

WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Jean-Michel Sama Lukonde, amejiuzulu wadhifa wake baada ya kukaa madarakani kwa miaka mitatu.

Lukonde, ametangaza kujiuzulu juzi kupitia video iliyotolewa na ofisi ya rais na kusambaa haraka katika mitandao ya kijamiii.

Shirika la habari la Reuters liliripoti kuwa Rais wa DRC, Felix Tshisekedi amekubali ombi la kujiuzulu kwa Lukonde.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa Rais Tshisekedi aliiomba serikali iliyoongozwa na Lukonde kuendelea na majukumu yake hadi serikali mpya itakapoundwa.

Katika katiba ya DRC, serikali inaongozwa na waziri mkuu.

Kutokana na uamuzi huo, Lukonde sasa atabaki kuwa mbunge baada ya uchaguzi uliofanyika Desemba mwaka jana aligombea nafasi hiyo na kufanikiwa kuchaguliwa kwa kura nyingi.

Lukonde aliteuliwa kuwa waziri mkuu mwaka wa 2021, akimrithi aliyekuwa kwenye nafasi hiyo Sylvestre Ilunga Ilunkamba, ambaye alijiuzulu baada ya wabunge kumpigia kura ya kutokuwa na imani naye.

Wakati huo huo, Baraza la Usalama la Umoja limewawekea vikwazo watu sita kutoka makundi matano yenye silaha yanayopigana mashariki mwa DRC.

Wakati vikwazo hivyo vinawekwa, mapigano makali yakizidi kushuhudiwa katika eneo hilo kati ya jeshi la serikali na waasi M23 wanaoungwa mkono na Rwanda.

Mapigano hayo yaliyodumu kwa miongo kadhaa, yameongeza hatari ya mzozo kati ya DRC na Rwanda.

Naibu Balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa, Robert Wood, amesema ni lazima DRC na Rwanda zijiepushe ma vita.

"Marekani inaunga mkono kwa dhati uhuru na uadilifu wa eneo la DRC na amani ya kudumu kwa raia wake. Rwanda na DRC lazima zirudi nyuma kutoka kwenye ukingo wa vita," alisema balozi Wood katika mkutano wa 15 wa Baraza la Usalama uliofanyika juzi.

Kamati ya vikwazo vya Baraza la Usalama kwa nchi ya DRC iliweka vikwazo vya silaha, kusafiri na kuzuiliwa kwa mali kwa viongozi wawili wa Allied Democratic Forces (ADF), kiongozi mmoja kutoka kundi lenye silaha la Twirwaneho na mmoja kutoka Muungano wa Kitaifa wa Umoja wa Watu wa Uhuru wa Congo (CNPSC). **BBC**




Balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa, Lind Thomas-Greenfield, akipiga kura ya turufu kupinga rasimu inayotaka kusitishwa mapigano Ukanda wa Gaza juzi. **PICHA: AP**

# Marekani yapiga kura ya turufu kuzuia usitishwaji wa mapigano

**NEWYORK,** MAREKANI

MAREKANI imetumia kura ya turufu kupinga azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lililotaka kusitishwa mapigano katika eneo hilo la Kipalestina la Ukanda wa Gaza.

Hata hivyo, ripoti kutoka Gaza inaeleza usiku wa jana eneo hilo liliendelea kukumbwa na mashambulizi kutoka vikosi vya jeshi la Israel.

Rasimu hiyo ambayo Marekani iliipinga kwa kura ya turufu ilitayarishwa na nchi ya Algeria, ambayo ilitaka kusitishwa mara moja kwa mapigano hayo kwa ajili ya kusaidia kupelekwa misaada ya kiutu na kuachiwa bila masharti mateka wote waliokamatwa katika shambulizi la Oktoba 7.

Balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa, Lind Thomas-Greenfield, alisema rasimu hiyo itaathiri mazungumzo yanayofanywa na pande zote kuhusu mpango wa kuwaachia mateka na kusitishwa mapigano angalau kwa wiki sita.

Katika taarifa yake, kundi la Hamas lilieleza kwamba kura hiyo ya turufu ya Marekani ni sawa na kutoa idhini kwa Israel kuendelea kufanya maangamizi zaidi.

Kura hiyo ilisababisha nchi kadhaa zikiwemo China, Urusi, Saudi Arabia, Ufaransa na Slovenia kuikosoa Marekani na kueleza masikitiko yao.

Wakati mvutano wa kidiplomasia ukiendelea, vikozi vya Israel viliongeza kasi ya kuishambulia Gaza kwa kutumia makombora ya angani na ardhini.

Katika mashambulizi hayo, yamesababisha vifo vya Wapalestina zaidi ya 103 katika kipindi cha saa 24.

Wizara ya Afya ya Gaza inayodhibitiwa na Hamas ilisema mashambulizi hayo ya usiku wa kuamkia Jamatano ulihusisha mji Rafah ambao ulimwengu wanapinga kushambuliwa.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) limesitisha shughuli za usambazaji wa chakula kaskazini mwa ukanda wa Gaza hadi pale hali ya usalama itakaporuhusu kuendelea kwa zoezi hilo. **DW**

# GEITA GOLD YALALAMIKA RATIBA LIGI KUU SI RAFIKI

**Na Oliver Albert**

BAADA ya timu yake kuchapwa mechi tatu mfululizo, Kocha Mkuu wa Geita Gold, Dennis Kitambi, amesema ratiba ngumu ya Ligi Kuu Tanzania Bara imechangia matokeo hayo.

Geita Gold ilianza kucheza na Simba nyumbani Februari 12, na kuchapwa bao 1-0, kisha ikasafiri hadi Dar es Salaam ilipocheza na Azam Februari 16 na kulala kwa mabao 2-1 na kugeuza kurudi Geita kuikabili Ihefu iliyocheza nayo Februari 19, mwaka huu na kufungwa mabao 2-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kitambi alisema walikuwa hawana muda wa kupumzika na kufanya mazoezi vizuri kwa sababu mechi zimekaribiana, hivyo kuwachosha wachezaji wake.

"Ratiba yetu ni ngumu sana kwa sababu kila baada ya siku mbili mnacheza mechi na wakati mwingine mnatakiwa kusafiri hivyo wachezaji wanachoka.

Ndio ratiba imeshapangwa hivyo lazima tupambane nayo hivyo hivyo kuhakikisha tunakuwa sawa na kuanza kupata matokeo mazuri, " alisema Kitambi na kuongeza ;

"Muhimu ni kusahihisha makosa katika michezo iliyopita hasa katika eneo la ulinzi ili mechi zijazo tuweze kushinda na kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi.

Geita Gold itashuka tena uwanjani Februari 25, mwaka huu kuikabili Mashujaa FC kwenye uwanja wao wa nyumbani wa Shule ya Sekondari Nyankumbu ulioko mkoani, Geita.

Timu hiyo iko katika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 16 baada ya kucheza michezo 16, imeshinda minne, imetoka sare michezo minne na kupoteza nane.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo wakiwa na pointi 43 wakifuatiwa na Azam FC yenye pointi 36 sawa na Simba lakini Wekundu wa Msimbazi wakiwa na mchezo mmoja pungufu.

Mtibwa Sugar yenye pointi nane ndio inaburuza mkia katika ligi hiyo yenye timu 16 wakati Coastal Union ya jijini, Tanga yenye pointi 23 inakamilisha 'Top Four'.



Wasanii za Bongo Movie kutoka Taasisi ya Mtandao wa Utamaduni na Sanaa Nchini (MMASUTA), wakiwa na viongozi wa Serikali ya Wilaya ya Morogoro baada ya kukabidhi misaada mbalimbali kwa ajili ya waathirika wa mafuriko yaliyotokea kwenye Manispaa ya Morogoro. **PICHA : ASHTON BALAIGWA**

# Wasanii watoa msaada Morogoro

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

WASANII wa filamu za Bongo Movie kutoka Taasisi ya Mtandao wa Utamaduni na Sanaa Tanzania (MMASUTA), wametoa misaada mbalimbali ikiwamo vyakula kwa waathirika wa mafuriko yaliyotokea katika Manispaa ya Morogoro na kusababisha vifo na kuwaacha wengine kukosa makazi.

Mafuriko hayo yalitokea katika Kata ya Bigwa, Kihonda, Lukobe na Mafisa yalitokana na mvua zilizonyesha kwenye maeneo mbalimbali mkoani hapa katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita.

Akizungumza wakati akikabidhi misaada hiyo kwa uongozi wa Serikali ya wilaya ya Morogoro, Mwenyekiti wa MMASUTA, David Msuya, alisema wasanii waliguswa na maafa hayo na kuona kuunga mkono familia zilizopatwa ka kadhia hiyo. Alisema mafuriko hayo yameleta changamoto nyingi kwa wananchi pamoja na watoto hivyo wameona ni vyema kusaidia ili kutatua baadhi ya changamoto ikiwa ni jitihada za kuunga mkono serikali.

Naye mwigizaji wa filamu wa mda mrefu Emanuel Kipawa 'Mfamaji' kutoka Kaole, amewataka wadau wengine mbalimbali hapa nchini wakiwemo wasanii wakubwa kusaidia waathirika hao wa mafuriko kwakuwa bado wanahitaji misaada zaidi ikiwemo baadhi yao kujengewa nyumba,vyakula na masuala ya kijamii.

Akipokea msaada huo, kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Ofisa Tawala, Janet Chacha, aliwashukuru wasanii hao kwa kuguswa na aliwahakikishia misaada hiyo itafika kwa walengwa huku akiwataka kuwashawishi wasanii wengine kuwasaidia wathirika hao wa mafuriko.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alikaririwa akisema watu 20 walifariki kutokana na mafuriko hayo.

## Timu za wanawake kikapu zaongezeka

**Na Oliver Albert**

WAKATI Ligi ya Kikapu Mkoa wa Dar es Salaam (BDL), ikitarajia kufanyika kuanzia Machi 2, mwaka huu, imeelezwa kuna ongezeko kubwa la timu za wanawake msimu huu.

Mwaka jana timu zilizoshiriki ligi hiyo zilikuwa nane tu lakini msimu huu jumla ya klabu 16 sawa na wanaume zitashiriki.

Timu zilizoshiriki mwaka jana ni Vijana Queens ambao waliibuka mabingwa, JKT Stars, UDSM Queens, Jeshi Stars, Ukonga Queens, Mchenga Queens, Polisi Stars na DB Lioness na zilizoongezeka ni City Queens, Kurasini Divas, Kigamboni Queens, Tausi Royals, Twalipo Queens, Mgulani Stars, Pazi Queens na DB TRoncatti.

Kamishina wa Wanawake wa Chama Cha Kikapu Dar es Salaam (BD), Fatma Yassoda, alisema wanafuraha kuona kuna mwitikio mkubwa wa watoto wa kike kucheza kikaou hivyo kufanya idadi ya timu kuongezeka kwenye ligi.

"Tulikuwa tunatamani timu za wanawake ziwe nyingi kwenye ligi na tunashukuru mwaka huu jambo hilo linaenda kufanikiwa. Uwepo wa timu nyingi kwenye ligi utaongeza ushindani na pia utaongeza fursa kwa watoto wa kike kuonekana, " alisema Yassoda.

## Kundemba, KVZ mechi ya kibabe

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Kundemba FC inatupa karata yake ya nne dhidi ya KVZ katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo huku wenyeji wakiwa hawana matokeo mazuri msimu huu.

Kundemba ipo katika nafasi ya 12 ikiwa na pointi 19, imecheza michezo 18 na kati ya hiyo imeshinda mitano, imetoka sare mara nne na imefungwa michezo tisa.

Akizungumza na Nipashe Kocha Mkuu wa Kundemba, Ali Vuai, alisema mipango yao ni kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ili kuibakisha timu hiyo kwenye Ligi Kuu Zanzibar.

"Hatukuanza vizuri msimu huu, na sio kama hatukufanya usajili mzuri hapana bali ni ushindani uliopo katika Ligi Kuu Zanzibar, kila timu ilijiandaa kuhakikisha haipotezi malengo na sisi pia tulijiandaa ila ni upepo tu mbaya ulikuwa upande wetu,"alisema Vuai.

Aliongeza wamejiandaa kukutana na upinzani kwa sababu wapinzani wao walipoteza mchezo uliopita, hivyo wataingia dimbani na mipango mipya ili kuondoka na alama tatu muhimu.

## ZISIKUPITE

### EDERSON AGEUKA LULU
KLABU ya Manchester United na Liverpool ni miongoni mwa timu kadhaa za Ligi Kuu England zinazomtaka kiungo wa kati wa Atalanta, Ederson, huku Arsenal, Newcastle United na Tottenham Hotspur pia zikimfuatilia Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 24. **(Gazzetta dello Sport)**

### JUVENTUS YAINGIA VITANI
JUVENTUS pia wanamtaka Ederson, lakini wababe hao wa Serie A wameamua kufanya usajili wa mchezaji mwenzake wa Atalanta, Teun Koopmeiners, kiungo wa kati wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 25, kuwa kipaumbele chao. **(Gazzetta dello Sport)**

### GUEHI ANUKIA LIVERPOOL
LIVERPOOL inavutiwa na beki wa Crystal Palace, Marc Guehi, mwenye umri wa miaka 23. **(Telegraph)**

### PSG YAMTAKA OSIMHEN
KLABU ya Paris St-Germain inamlenga mshambuliaji wa Napoli mwenye umri wa miaka 25, Victor Osimhen, mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford (26) na kiungo wa kati wa Barcelona (19), Gavi msimu huu. **(I)**

### BREMER ATAJWA UNITED
KLABU ya Manchester United inavutiwa na mlinzi wa Juventus na Brazil mwenye umri wa miaka 26, Gleison Bremer, ambaye thamani yake ni euro milioni 70. **(Calciomercato)**

### FULHAM KUMUUZA PALHINHA
MAKAMU Mwenyekiti wa Fulham, Tony Khan, amesema klabu itazingatia ofa ambazo „zina maana" kwa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Palhinha, mwenye umri wa miaka 28. **(Sports)**

### KANE ATAKIWA UNITED
KLABU ya Manchester United inafikiria kurejesha nia yao ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa Bayern Munich, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 30 na kiungo wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong (26), msimu huu. **(Football Transfers)**

### GLOUKH AGOMBEWA ENGLAND
ASTON Villa inajiandaa kufungua zabuni ya kumnunua kiungo wa Red Bull Salzburg, Oscar Gloukh, raia wa Israel mwenye umri wa miaka 19 ambaye anazivutia Manchester United, Arsenal, Liverpool, Newcastle United na Barcelona - kwa ofa ya euro milioni 20. **(Ekrem Konur)**

### KLABU ZAMGOMBEA MORRISON
KLABU za Sheffield Wednesday, Bolton Wanderers na Peterborough United zinawania kumnunua kiungo wa kati wa Jamaica, Ravel Morrison, mwenye umri wa miaka 31, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka DC United inayoshiriki Ligi Kuu ya Soka ya Marekani. **(TeamTalks)**

### ZERBI ATAJWA BARCA
RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, ameomba ripoti zaidi za uchunguzi kuhusu Roberto de Zerbi, anapofikiria kumkaribia bosi wa Brighton ili kumrithi Xavi kama kocha mwishoni mwa msimu huu. **(Sport)**

### LONG ANUKIA MAREKANI
MLINZI wa Birmingham na Jamhuri ya Ireland, Kevin Long, mwenye umri wa miaka 33, anakaribia kukamilisha uhamisho wa kwenda Toronto FC ya Ligi Kuu ya Soka ya Marekani (MLS). **(Birmingham mail)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND 'AMEWAJIBU' WAKOSOAJI - GUARDIOLA

**Ni baada ya kufunga bao pekee na kuipa Manchester City...**

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesema, Erling Haaland, aliwafunga mdomo wakosoaji wake kwa kufunga bao pekee katika ushindi wa bao 1-0 wa Manchester City ilipoivaa Brentford, juzi.

Haaland alikuwa na majaribio tisa bila kufunga bao katika sare ya 1-1 dhidi ya Chelsea Jumamosi iliyopita na akakosa nafasi ya dhahabu kwa bao la kichwa kipindi cha pili.

Lakini katika mechi dhidi ya Brentford, mshambuliaji huyo wa Norway, ambaye bibi yake aliaga dunia wiki iliyopita, alifunga bao lake la 22 msimu huu na kuipa City ushindi na kupunguza pengo dhidi ya vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool.

„Mfungaji bora, mshambuliaji bora, anafunga mabao mengi, usimkosoe atakufunga mdomo," alisema Guardiola.

„Alikuwa nje kwa miezi miwili, alimpoteza bibi yake, si rahisi kwa mwanadamu. Katika aina hii ya mchezo kama Brentford, unamhitaji Erling."

City walipiga mashuti 31 dhidi ya Chelsea na mengine 25 dhidi ya Brentford kwa jumla ya mabao mawili. Ilionekana usiku wa kufadhaisha dhidi ya kikosi cha Thomas Frank kabla ya beki, Kristoffer Ajer, kuteleza katikati ya kipindi cha pili na kumruhusu Haaland kukimbilia pasi ya Julian Álvarez na kufunga bao la ushindi.

„Nadhani katika mchezo wote tulikuwa kiwango bora," alisema Frank.

„Ninajivunia sana na kufurahishwa na uchezaji wa wachezaji. Waliamini na inanipa imani kubwa kwao kwenda mbele.

„Kama asingeteleza nina hakika lisingekuwa bao. Haaland ni mwepesi lakini Kristoffer ni mwepesi vile vile."

Wakati huohuo, Guardiola alifichua baadaye Kevin De Bruyne aliachwa kwenye benchi dhidi ya Brentford baada ya kutojisikia vizuri kwenye misuli yake ya paja.

Kiungo huyo alikosa miezi mitano baada ya kufanyiwa upasuaji wa nyama ya paja na ingawa alitajwa kwenye benchi Jumanne, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 hakuweza kucheza.

„Leo(juzi) hatukuweza kumtumia Kevin kwa sababu alikuwa anasumbuliwa na misuli ya paja na sikutaka kujihatarisha," alisema Guardiola.

„Yuko sawa. Tahadhari tu kwa sababu hakujisikia vizuri na baada ya mapumziko ya miezi mitano hatukuchukua hatari yoyote."

HABARI MICHEZO

# DE JONG AKERWA TETESI HATIMA YAKE BARCELONA

**BARCELONA, Hispania**

KIUNGO wa kati wa Barcelona, Frenkie de Jong, amesema amekasirishwa na kukerwa na „uongo" unaozungumzwa kuhusu mustakabali wake.

De Jong mwenye umri wa miaka 26, amekuwa akipamba vyombo vya habari katika miezi ya hivi karibuni, kwa madai anaweza kuondoka Barca msimu huu wa joto huku klabu hiyo ikitafuta kuondoa mshahara wake kutoka kwenye bili yao.

Hata hivyo, mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi, ambaye ana mkataba hadi mwaka 2026, alisisitiza bado ana furaha katika klabu hiyo ya Katalunya na anakenrwa na habari zinazosambazwa na vyonbo vya habari.

„Nina hasira kidogo na kile wanahabari wanaandika kwa ujumla," alisema De Jong katika mkutano na waandishi wa habari kabla ya mchezo wa jana Jumatano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Napoli.

"Mambo mengi ambayo si ya kweli yametokea, sielewi, watu wanaripoti uongo, inanikera kidogo.

„Kwa mfano, vyombo vya habari vinazungumza mengi kuhusu mkataba wangu, mshahara wangu, uongo ni mwingi, ninapata euro milioni 40 au zaidi.

"Hiyo ni mbali sana na kile ninachopata, sitasema namba, lakini habari hizi sio za kweli.

„Vyombo vya habari lazima vibadilishe wanachofanya kwa makocha na wachezaji wengi, kwa sababu mnaandika vitu na kubuni vitu ambavyo si vya kweli.

„Nina furaha sana Barca, nimekuwa nikisema kila mara. Hii ndiyo klabu ya ndoto zangu, natumai nitacheza hapa kwa miaka mingi zaidi."

De Jong alijiunga na Barca kutoka Ajax mwaka 2019 kwa dau la awali la euro milioni 75 na amefanikiwa kuichezea klabu hiyo zaidi ya mechi 200.




## Jota kuigharimu Liverpool

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amesema hawezi kutoa muda kuhusu jeraha la Diogo Jota, lakini akasema fowadi huyo wa Liverpool atakuwa nje kwa „miezi kadhaa".

Jota alitolewa nje ya uwanja katika kipindi cha kwanza cha ushindi wa Liverpool dhidi ya Brentford Jumamosi iliyopita baada ya Christian Norgaard kutua kwa nguvu kwenye mguu wake.

„Kwa Diogo itachukua miezi sio wiki," alisema Klopp katika mkutano na waandishi wa habari.

„Sitaweza kusema muda hata kama ningetaka. Hivyo ndivyo ilivyo. Usipokuwa na wachezaji hawa haina maana."

Jeraha la Jota linakuja kama pigo kwa Liverpool, ambao wameegemea zaidi kwa Mreno huyo wakati Mohamed Salah hayupo.

Katika mechi 28 katika mashindano yote msimu huu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 amechangia mabao 18.

Utambuzi huo unamaanisha kuwa Jota ataungana na Trent Alexander-Arnold kwenye orodha ya wasiohudhuria katika fainali ya Kombe la Carabao dhidi ya Chelsea Jumapili.

Curtis Jones pia yupo shakani kucheza fainali hiyo pale kwenye Uwanja wa Wembley, baada ya kutolewa mapema kipindi cha kwanza dhidi ya Brentford kutokana na jeraha.




## Ratcliffe rasmi ndani ya United

**MANCHESTER, England**



KLABU ya Manchester United imethibitisha ununuzi wa hisa wa Sir Jim Ratcliffe wa asilimia 25 sasa umekamilika.

Ratcliffe alipata idhini ya Bodi ya Ligi Kuu England wiki iliyopita pamoja na Chama cha Soka England (FA), na sasa Ratcliffe na Kampuni ya INEOS wako huru kuanza kazi Old Trafford.

„Kuwa mmiliki mwenza wa Manchester United ni heshima kubwa na inakuja na jukumu kubwa," alisema Ratcliffe katika taarifa yake.

„Hii ni alama ya kukamilika kwa shughuli hiyo, lakini ni mwanzo tu wa safari yetu ya kuirejesha Manchester United kileleni mwa soka la England, Ulaya na duniani, tukiwa na vifaa vya hali ya juu kwa mashabiki wetu. Kazi ya kufikia malengo hayo itaongezeka kuanzia sasa."

Mwenyekiti Mwenza, Joel Glazer aliongeza: „Ningependa kumkaribisha Sir Jim kama mmiliki mwenza na ninatarajia kufanya kazi kwa karibu naye na INEOS Sport ili kuleta mustakabali mzuri wa Manchester United."

Kama sehemu ya makubaliano yake na Glazers, ambao wamebakia Old Trafford, Ratcliffe atachukua udhibiti wa shughuli zote za soka.

Kazi ya kutimiza maono yake tayari inaendelea, huku United ikifuata mpango ulioandaliwa na bosi huyo mpya wakati wa dirisha la usajili la Januari.

Nyuma ya pazia, United pia imekuwa ikirekebisha chumba chao cha bodi. Omar Berrada aliajiriwa kama mtendaji mkuu mpya, wakati mkurugenzi mpya wa michezo pia yuko njiani.

Makubaliano yamefikiwa na Dan Ashworth wa Newcastle United, lakini Magpies hao wanataka ada kubwa ya fidia ii kumwachia.

HABARI MICHEZO

# BABU : WADAU ZITUMIENI FURSA KILI MARATHON 2024

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, ametoa rai kwa wakazi wa mkoa huo hususan wafanyabiashara kutumia fursa za kibiashara zinazotokana na mbio za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon.

Babu alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza kuhusiana na maandalizi ya mbio hizo kwa upande wa serikali ya mkoa.

"Mbio hizi zinatarajiwa kuhusisha zaidi ya washiriki 10,000 na idadi kama hiyo ya watu wengine watakaokuja mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya kufuatilia mbio hizo muhimu Afrika Mashariki," alisema na kuongeza;

Taarifa nilizonazo tayari nyumba za kulala wageni zote zimejaa hapa Moshi Mjini, maeneo mengine yaliyoko nje ya Moshi Mjini na wengine wamechukua vyumba mkoa wa jirani wa Arusha,".

Aidha Babu aliwapongeza wandaaji wa mbio hizo ambapo alisema mbali na kuinua vipaji vya wanamichezo katika tasnia ya riadha, pamoja na kukuza uchumi wa koa na ule wa Taifa, pia mbio hizo zinaunga mkono juhudi za Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, zinazolenga kukuza sekta ya michezo nchini.

Kuhusu maandalizi kwa ngazi ya Mkoa, Babu alisema yote yanaenda vizuri ikiwamo suala la usalama kwa washiriki na wageni wote watakaofika Moshi.

Aliushukuru waandaji kwa kutoa fursa kwa uongozi wa mkoa kuandaa jogging maalum itakayofanyika Feburuari 24, mwaka huu ambayo itakuwa ni ‚kipasha moto' kwa ajili ya mbio zitakazofanyika Jumapili.

Meneja wa Bia ya Kilimanjaro, Catherine Lyakurwa, alisema maandalizi yamefikia pazuri na washiriki wajiandae kupata burudani ya aina yake.

Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo, alisema udhamini wao kwa miaka tisa umekuwa na tija kubwa sana.

„Safari hii tutafunga WIFI katika vituo mbalimbali Moshi Mjini na itakuwa bure kwa kila mtu,"alisema Kinabo.

Wadhamini wengine wa mbio hizo ni Mexa za maji- Simba Cement, TPC Sugar, CRDB Bank, Kilimanjaro Water, wabia wakuu- GardaWorld Tanzania, Salinero Hotel naCMC Automobiles na Wasambazaji wakuu hoteli ya Keys na Kibo Palace.




Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu (kulia), akipokea fulana kwa ajili ya kushiriki mbio za Kili Marathon kutoka kwa Meneja Matukio wa Kilimanjaro Premium Lager International Marathon 2024, David Marealle (kushoto). Katikati ni Meneja wa Itifaki wa mbio hizo, Nurdin Saggafu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dodoma Jiji yatambia nyumbani

**Na Adam Fungamwango**

Dodoma Jiji FC imesema inafurahishwa na mafanikio waliyoyapata kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwamo kupoteza mechi moja tu kwenye uwanja wa nyumbani.

Ofisa Habari wa Dodoma Jiji, Patrick Shemindu, alisema malengo makuu msimu huu ni kumaliza katika nafasi nne za juu na dalili zimeshaanza kuonekana kutokana na kuwa moja kati ya timu chache ambazo zimetumia vyema ardhi ya nyumbani.

„Timu yenye malengo ya kushika nafasi nne za juu utaiona hata kwenye matokeo yake ya mechi za nyumbani, sisi tumepoteza mechi moja tu tukicheza nyumbani dhidi ya Singida Fountain Gate, tofauti na hapo tumeshinda na kutoa sare, hii inaonyesha tumefanya vizuri sana katika mzunguko wa kwanza, na tunaahidi tutafanya vyema sana mzunguko wa pili," alisema ofisa huyo.

Aliongeza mara nyingi timu inayotaka kutwaa ubingwa huwa ina viashiria vyake, inayotaka nafasi ya nne pia ina viashiria ambavyo ni kama walivyonavyo, ikiwapo kutopoteza pointi tatu kirahisi ukiwa nyumbani.

Dodoma jiji imecheza mechi saba nyumbani, ikishinda tatu, sare tatu na kupoteza mechi moja mpaka sasa, iko nafasi ya tisa ikiwa na pointi 19.

## Awesu rasmi atajwa katika rada za Yanga

INATOKA UK. 24

ana basi hana mashaka kwa sababu kazi yake ni kucheza mpira na atakuwa tayari kujiunga na Yanga au klabu yoyote ambayo wataafikiana na uongozi wa timu yake.

"Unajua kwangu ni faraja kubwa sana kuona kiongozi wa Yanga akinizungumzia, ubora wa kazi yangu unaonekana naamini huu ndio mwanzo mwingine wa safari yangu ya soka.

Bado nina mkataba hadi 2025, suala la kupendekeza jina langu kwa uongozi na benchi la ufundi kuwa sehemu ya nyota watakaowasajili hilo ni jambo zuri, lakini kwa sasa naheshimu mkataba wangu," alisema Awesu.

Aliongeza mafanikio ni jitihada za mchezaji mwenyewe inatakiwa kupambana kwa ajili ya timu la sivyo wachezaji wakigeni watakuwa wanasajili kila kukicha.

Gamondi alisema anajivunia wachezaji wake kuonyesha uwezo mkubwa katika kila mechi na hii inaonyesha wanafuata vyema yale anayowapa kwenye uwanja wa mazoezi.

Alisema anaanza kuona washambuliaji wake wanafunga kama ilivyo kwa Guede, huku akimwambia asiwe na presha kwa sababu atafunga mabao mengi kutokana na mfumo ambao anataka kuutumia.

Aliongeza awali walipata mabao kupitia viungo hali imeanza kubadilika kwa kutumia mawinga imesababisha Guede kufunga magoli mawili katika mchezo huo wa FA.

"Kuhusu kutengeneza nafasi tunazipata nyingi, ukiangalia mechi ya Morogoro tulitengeneza nafasi zaidi ya 10 lakini tukapata mabao matatu, ninaimani tutaendelea kutengeneza nafasi na kutumia katika mechi zijazo kufunga idadi ya mabao mengi," alisema kocha huyo.

Kuhusu maandalizi ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CR Belouizdad, Gamondi, alisema wanatarajia kufanya vizuri katika mchezo huo kwa sababu malengo yao ni kusonga mbele.

"Utaratibu wangu ninafanya maandalizi hatua kwa hatua, baada ya mechi hii (Polisi Tanzania), tunarejea uwanjani kujiandaa na mchezo dhidi ya CR Belouizdad. Tulitaka kufuzu hatua ya makundi tukafanikiwa baada ya miaka mingi na sasa tunataka kutafuta matokeo mazuri yenye ushindi mkubwa ili mwisho wa siku tukacheza robo fainali, " Gamondi aliongeza.

Guede alisema anafurahi kuona amefunga mabao mawili ikiwa ni mara ya kwanza na anaimani sasa amezaliwa upya na atahakikisha anaendelea kupambania timu yake kupata matokeo mazuri.

Michezo
Alhamisi Februari 22, 2024
Nipashe

## Ratcliffe rasmi ndani ya Man United

UKURASA 22



# AWESU RASMI ATAJWA KATIKA RADA ZA YANGA

### ●●●Gamondi afunguka kiwango cha Guede kimempagawisha, anaamini...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI kumtaja kiungo wa KMC FC, Awesu Awesu ametajwa kuwa katika rada za Yanga, Kocha Mkuu wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Miguel Gamondi, amefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na straika wake, Joseph Guede.

Straika huyo raia wa Ghana alifungua akaunti yake ya mabao mawili Yanga ikipata ushindi wa magoli 5-0 katika mechi ya michuano ya Kombe la FA dhidi ya Polisi Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, aliliambia Nipashe Awesu yuko katika mipango ya timu yao kuelekea dirisha 'kubwa' la usajili litakalofunguliwa baadaye mwaka huu.

Kamwe alisema wakati umefika kwa Awesu kutoka KMC na kujiunga na timu 'kubwa' kutokana na uwezo aliokuwa nao katika kucheza soka.

Ofisa huyo aliendа mbali na kusema ikitokea Yanga watahitaji kiungo wa ndani, kiungo huyo atakuwa sehemu ya mipango ya usajili wao kwa kuushawishi uongozi kumnasa kutokana na kiwango bora alichonacho.

Naye Awesu alisema amefurahi kusikia kauli hiyo ya kuhusishwa na Yanga na kuongeza ni lazima kufanyike makubaliano rasmi ya pande zote tatu lakini upande wake hana tatizo.

Awesu alisema endapo Yanga na KMC zitakubali-

INAENDELEA UK. 23



Guede

## Benchikha aanika 'siri' itayowabeba

**Na Adam Fungamwango**

ZIKIWA zimebakia saa chache kabla ya kuwavaa wenyeji Asec Mimosa, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, amewaambia wachezaji wake mbinu pekee ya kushinda mechi ya kesho ni kuzidisha umakini wanapokuwa na mpira, kutokuwa na presha.

Simba itashuka kwenye Uwanja wa Felix Houphouet Boigny, jijini Abidjan, Ivory Coast kuanzia saa 4:00 usiku kuwakabili wenyeji katika mechi ya raundi ya tano ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku ikihitaji ushindi ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kutinga hatua ya robo fainali.

Benchikha amewaambia wachezaji wake ili kuhakikisha wanavuna matokeo chanya, wanatakiwa kuepuka kufanya makosa ya binafsi na ya kitimu.

Kocha huyo alisema kiufundi ni ngumu kucheza na timu ambayo haina presha na imeshatimiza malengo yake kwa sababu hawaogopi kufanya makosa uwanjani, badala yake wachezaji wa Simba ndiyo wanatakiwa kuongeza umakini.

"Ni mechi ngumu kiufundi kwa sababu tunacheza na timu ambayo haina presha, imetulia na haina wasiwasi na matokeo yoyote yatakayotokea, imeshatimiza malengo yake ya kutinga hatua ya robo fainali, kucheza na timu ya aina hii ni tabu sana," alisema Benchikha, raia wa Algeria.

Aliongeza amewataka wachezaji wake wawe watulivu na kuhakikisha hawapotezi mipira kirahisi ili kujiweka katika mazingira ya kutawala mchezo lakini pia kujitahidi kupunguza makosa.

Naye Meneja Habari na Mawasiliano na klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema tangu walipofika Ivory Coast hakuna figisu yoyote waliyokutana nayo, na ametamba Asec Mimosas haina ubavu wa kuifanyia Simba vitu vya 'hujuma' ingawa wamechukua tahadhari zote.

Alisema mchezo wa kesho utakuwa ni wa nyota tano kwa sababu Asec Mimosas ni timu bora, lakini kwao watashuka 'kufa na kupona' kusaka matokeo ya ushindi peke.

Mratibu wa Simba, Abbas Ally, mbali na kusema hali ya hewa ya jiji hilo haina tofauti ya ya Dar es Salaam, inaonekana mashabiki wa soka nchini humo ni kama wamestukizwa kwa sababu bado walikuwa na furaha ya timu ya taifa kutwaa ubingwa wa Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON).

"Hapa wanachozungumzia ni mafanikio wa timu yao kutwaa Kombe la AFCON, na mechi hii ni kama imewashtukiza, walikuwa wamesahau hivi, furaha ilikuwa imewazidi na hawakujua kama mechi ya Ligi ya Mabingwa itapigwa mapema hivi japo ratiba ilishapangwa kitambo," alisema mratibu huyo.



Manula

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >